JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2017/18

APRILI, 2017

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2017/18

## A. UTANGULIZI

1. *Mheshimiwa Spika,* naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33), Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi (Fungu 06), Ushauri wa Mafuta na Gesi (Fungu 11), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67), Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 09), na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04). Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

2. *Mheshimiwa Spika,* Kwanza namshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuniamini katika nafasi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; ninamuahidi kuwa nitaendelea kutekeleza wajibu wangu kwa ufanisi wa hali ya juu na uadilifu. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Vyama vya Wafanyakazi na Wafanyakazi kwa ujumla kwa kuendelea kunipatia ushirikiano ninapoendelea kuwawakilisha. Vilevile, naishukuru familia yangu kwa dhati ya moyo wangu kwa ushirikiano wanaonipatia na kuwa wavumilivu ninapotekeleza majukumu yangu.

3. *Mheshimiwa Spika,* naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jasson Samson Rwekiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini na Makamu wake Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchema, Mbunge wa Viti Maalum Tabora Mjini kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2016/17 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Maoni na ushauri wa Kamati hiyo umetuwezesha na utaendelea kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi.

4. *Mheshimiwa Spika,* kwa namna ya pekee, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri unaohimiza uadilifu, uwajibikaji na utendaji wenye matokeo katika Utumishi wa Umma. Aidha, namponge kwa uamuzi wake wa kijasiri wa kuhamishia Serikali Dodoma, uamuzi ambao ulikuwa mgumu kufanyika kwa zaidi ya miaka arobaini. Pili, nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

5. *Mheshimiwa Spika,* Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, kwa uongozi wake shupavu wa Serikali ya Zanzibar na nia yake thabiti ya kuleta maendeleo Zanzibar. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa moyo wake wote.

6. *Mheshimiwa Spika,* napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuwa nguzo muhimu ya utekelezaji, usimamiaji na uratibu wa kazi za kila siku

za Serikali na kuwa Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni. Aidha, nampongeza kwa kusimamia vizuri utekelezaji wa uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma kwa awamu.

7. *Mheshimiwa Spika,* naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara na hekima. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa umahiri na kazi nzuri wanayoifanya ya kuliongoza Bunge lako Tukufu.

8. *Mheshimiwa Spika,* Nawapongeza pia Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa mafanikio wanayoendelea kuyapata katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Kwa namna ya pekee, nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Naibu wake Mheshimiwa Selemani Said Jafo (Mb), kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais.

9. *Mheshimiwa Spika*, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Rais ambao ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Kabudi (Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria) kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa msiba wa Mbunge Mheshimiwa Dkt. Elly Macha, tunaomba Mola aiweke roho ya marehemu pema peponi, Amina!

10. *Mheshimiwa Spika,* nawashukuru Balozi John William Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana Alphayo Japani Kidata, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Dkt. Laurean J. Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Bi. Susan Paul Mlawi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Makamishna, Watendaji Wakuu wa Tume na Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote kwa kazi nzuri wanazozifanya katika

kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati.

11. *Mheshimiwa Spika,* kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kushukuru na kuwataja wachache ambao ni:- China, Japan, Uingereza, India, Korea ya Kusini, Ujerumani, Canada, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Denmark, Norway, Uholanzi, Finland, Uswisi, Indonesia, Brazil, Italia, Malaysia, Misri, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubelgiji, Ireland, Israel. Vilevile, nashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia, OFID-OPEC Fund for International Development, Japan (JICA), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Japan (Japanese Social Development Fund), DfID, KOICA, GIZ, DFATD, USAID, SIDA, UNDP, Jumuiya ya Madola, DANIDA, NORAD na Taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation.

12. *Mheshimiwa Spika,* mwisho kabisa ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Watumishi wote wa Umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi mkubwa, uzalendo wao, ari yao na imani yao kwa Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli; hayo yamewezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi.

13. *Mheshimiwa Spika,* naomba kulithibitishia Bunge lako tukufu kwamba Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaendelea kutekeleza maelekezo yaliyotolewa katika hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akifungua Bunge la 11 yaliyohusu kupunguza urasimu ili kuongeza kasi ya utekelezaji, kubana matumizi na kurejesha nidhamu ya Serikali na Utumishi wa Umma kwa kuongeza uwazi na kusimamia sheria, kanuni na taratibu za uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma ili wawajibike kwa wananchi ambao ndio wateja na waajiri wakuu wa watumishi wa umma. Vilevile, tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais katika vita

dhidi ya rushwa, ubadhirifu, ufisadi, uzembe, uvivu, ukiukwaji wa maadili na utumishi hewa kwa kuwawajibisha wanaodhihirika kujihusisha na vitendo hivyo. Hatua anazoendelea kuchukua Mheshimiwa Rais zinatakiwa kuungwa mkono na Bunge lako Tukufu pamoja na wale wote wanaoitakia mema nchi yetu. Dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na Serikali inayowahudumia wananchi wa kawaida itatimia kwa Watumishi wa Umma wote kufanya kazi kwa juhudi, maarifa na uadilifu mkubwa. Tunaendelea kusisitiza utoaji wa huduma bora, kwa haraka na kwa staha ili kuwaondolea wananchi usumbufu.

14. *Mheshimiwa Spika,* kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Watanzania wenzetu waliopotelewa na ndugu zao kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hiki yakiwemo Tetemeko lililotokea Mkoa wa Kagera, ajali na mafuriko yaliyotokea katika sehemu mbalimbali nchini. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema, peponi. Amina.

15. *Mheshimiwa Spika,* hotuba yangu itazungumzia maeneo makuu mawili ambayo ni: Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 pamoja na Mpango wa Utekelezaji na Maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA WA 2016/17

16. *Mheshimiwa Spika,* utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa 2016/17 ulizingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015. Shughuli zilizotekelezwa na kila Taasisi ni kama ifuatavyo:-

### OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

17. *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Fungu:20 Ofisi ya Rais, Ikulu liliidhinishiwa Shilingi

14,962,054,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2017 Shilingi 11,063,163,664 zilipokelewa na kutumika.

OFISI YA RAIS NA SEKRETARIETI YA BARAZA LA MAWAZIRI

18. *Mheshimiwa Spika,* ili kutekeleza majukumu yake, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri (Fungu 30) linalojumuisha Taasisi zilizo chini ya Ikulu, liliidhinishiwa Shilingi 793,164,600,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 362,715,571,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 430,449,029,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2017 Shilingi 547,583,679,331 zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo Shilingi 260,648,784,846 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 286,934,894,485 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

(a) Ikulu

19. *Mheshimiwa Spika,* Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Huduma kwa Rais na familia yake ziliendelea kutolewa;

(ii) Huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya uchumi, siasa, masuala ya jamii, sheria, mawasiliano na habari kwa umma, uhusiano wa kimataifa na maeneo mengine zilitolewa kwa ajili ya kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

(iii) Mikutano 31 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika, ambapo nyaraka 49 zilichambuliwa. Mikutano 17 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika na nyaraka 26 zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Mikutano 9 ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka 28 zilijadiliwa na kufanyiwa maamuzi. Aidha, mikutano 14 ya kazi ya Makatibu Wakuu ilifanyika na mada mbalimbali ziliwasilishwa na kujadiliwa;

(iv) Mkutano wa Tathmini wa Mwaka kati ya Wakurugenzi wa Sera na Mipango/Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri kwenye Wizara na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ulifanyika tarehe 13-17 Februari, 2017, Dodoma. Katika Mkutano huo, Taasisi ya Uongozi ilitoa mafunzo yaliyohusu masuala ya uongozi na uchambuzi wa sera. Aidha, mafunzo kuhusu maandalizi ya Nyaraka mbalimbali za Baraza la Mawaziri yalitolewa;

(v) Hotuba 18 za Mheshimiwa Rais zilichapishwa na kutangazwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari nchini. Aidha, Vipindi Maalum vya Televisheni 24 vinavyojulikana kwa jina la "Makala ya Rais" vilitengenezwa na kurushwa hewani kwenye vyombo mbalimbali vya habari;

(vi) Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa, Awamu ya Tatu (2016–2022) ulizinduliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 10 Desemba, 2016 katika Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Duniani;

(vii) Vikao 5 vya Kamati ya Taifa ya Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP) vilifanyika kwa ajili ya kutathmini utekelezaji wa Mpango Kazi wa OGP. Aidha, warsha ya wadau ya kujadili na kutoa maoni kuhusu Mpango huo ilifanyika mwezi Septemba, 2016, Dar es Salaam;

(viii) Rufaa 101 za Watumishi wa Umma na Mamlaka za Nidhamu zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa uamuzi ambapo kati ya hizo, Rufaa 89 zilitolewa uamuzi na wahusika kujulishwa. Aidha, malalamiko 600 ya Watumishi wa Umma na wananchi wengine yalichambuliwa na kutolewa maelekezo;

(ix) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ilishiriki katika kutoa majibu na ushahidi kwenye kesi za madai 8 zinazohusu Watumishi wa Umma na wananchi wengine zilizoko Mahakama Kuu dhidi ya uamuzi wa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Katibu Mkuu Kiongozi;

(x) Vikao 4 vya uratibu na uendeshaji wa maboresho chini ya Katibu Mkuu Kiongozi kujadili mafanikio, changamoto na mipango ya baadae ya maboresho vilifanyika;

(xi) Ufuatiliaji wa mifumo iliyosimikwa na Programu za Maboresho katika Ngazi za Wizara na Mikoa ya Shinyanga na Simiyu ulifanyika;

(xii) Zahanati ya Ikulu imetoa matibabu kwa watumishi 1,466. Kati ya hao, wanaume ni 847 na wanawake 619. Aidha, Watumishi wa Zahanati walifanya ziara katika Ikulu Ndogo 9 na kufanya upimaji wa afya za Watumishi na familia zao na kutoa ushauri nasaha. Ikulu Ndogo zilizotembelewa ni Chamwino, Dodoma, Mwanza, Lushoto, Tabora, Shinyanga, Arusha, Moshi na Tabora;

(xiii) Watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI na familia zao wamepata huduma muhimu za dawa, lishe na ushauri nasaha kupitia Zahanati ya Ikulu; na

(xiv) Ufuatiliaji na ukaguzi wa Miradi ya TASAF na MKURABITA umefanyika katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Morogoro, Dodoma pamoja na Unguja na Pemba. Aidha, miradi ya utoaji wa mikopo kwa vijana na wanawake inayotekelezwa na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea katika Mikoa ya Njombe miradi 4 na Morogoro miradi 3 ilikaguliwa.

(b) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)

20. *Mheshimiwa Spika,* TAKUKURU imeendelea kutekeleza jukumu lake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329, ambalo ni kuelimisha umma kuhusu athari za rushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa,

kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya Sheria na kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya rushwa. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Uchunguzi wa majalada 376 ulikamilika na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya kuombewa kibali cha kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani. Majalada 157 kati ya yaliyopelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani;

(ii) Kesi 706 ziliendeshwa mahakamani zikiwemo kesi mpya 227. Katika kipindi hiki, kesi 264 ziliamuliwa mahakamani ambapo kati ya hizo, kesi 161 watuhumiwa wake waliachiwa huru na kesi 103 watuhumiwa wake walipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo au kulipa faini. Aidha, kesi 33 ziliondolewa mahakamani kutokana na sababu mbalimbali. Kesi 409 zinaendelea mahakamani;

(iii) Shilingi bilioni 12.316 ziliokolewa kutokana na operesheni zilizofanywa na TAKUKURU na kurejeshwa Serikalini. Kati ya fedha zilizookolewa, Shilingi bilioni 8.009 zilitokana na ukwepaji ushuru (EFDs), Shilingi bilioni 2.6 zilitokana na ubadhirifu, Shilingi milioni 912.396 zilitokana na mishahara hewa na Shilingi milioni 794.182 ziliokolewa kutoka katika maeneo mengine. Aidha, nguvu kubwa imeelekezwa kudhibiti rushwa katika eneo la ukusanyaji mapato ya Serikali, uzuiaji wa malipo hewa na ukaguzi wa miradi ya maendeleo;

(iv) Kutokana na kuimarika kwa Kitengo cha ufuatiliaji na urejeshaji wa mali, TAKUKURU imefanikiwa kutaifisha nyumba 6 ambapo 5 ziko Buhongwa na moja iko Ilemela Mkoani Mwanza pamoja na magari 4 ambayo ni Toyota Chaser 2, Toyota Land Cruiser 1 na Mitsubishi Fuso 1 zilizopatikana kwa njia ya rushwa;

(v) Utafiti wenye lengo la kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mianya ya rushwa katika Sekta za Uhamiaji na Afya umefanyika. Kazi hizo ni uchambuzi wa mianya ya rushwa katika mfumo wa utoaji wa hati za kusafiria na tathmini ya uzingatiaji wa sheria na kanuni za uanzishaji na usimamizi wa maduka ya dawa muhimu;

(vi) Kazi 246 za uchambuzi wa mifumo na warsha/vikao 106 vya wadau kujadili matokeo ya kazi za utafiti na uchambuzi wa mifumo kwa lengo la kuweka mikakati ya kudhibiti rushwa vilifanyika katika maeneo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kilimo, Mifugo, Uchukuzi, Ardhi, Ujenzi, Mahakama, Biashara, Huduma za jamii, Fedha, Afya, Maji, Madini, Viwanda, Misitu, Nishati na Elimu. Aidha, kazi 18 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio yatokanayo na mapendekezo ya uchambuzi wa mifumo zilifanyika;

(vii) Elimu kuhusu athari za rushwa ilitolewa kupitia njia mbalimbali zikiwemo semina 1,912, mikutano ya hadhara/mijadala ya wazi 1,297, vipindi vya redio na televisheni 168, vipindi vya televisheni 8, maonesho 125 na taarifa kwa umma 57 zilitolewa kupitia vyombo vya habari. Aidha, habari/makala 185 ziliandaliwa kwa ajili ya wavuti na nakala za machapisho 16,000 zilisambazwa. Katika uelimishaji huo, wananchi 476,944 walifikiwa ana kwa ana. Idadi hiyo haihusishi waliofikiwa kwa njia ya redio, runinga na machapisho;

(viii) Kundi la vijana limeendelea kuwa ajenda muhimu ambapo vijana walio shuleni, vyuoni na walio nje ya shule walipatiwa elimu kuhusu rushwa na kuwasisitiza kujiunga na klabu za wapinga rushwa kwa lengo la kuwajenga kimaadili. Klabu mpya za wapinga rushwa 291 zilifunguliwa na 1,560 ziliimarishwa;

(ix) Kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Umma, TAKUKURU ilishiriki katika maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za

Binadamu Kitaifa. Kauli mbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa kujenga na kukuza maadili, haki za binadamu, uwajibikaji, utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa ambapo wananchi walipata fursa ya kufahamishwa mambo mbalimbali kupitia midahalo, matembezi ya hiari na wiki ya kuwapatia huduma wananchi;

(x) Kampeni ya Longa Nasi iliyobuniwa kuwahamasisha wananchi kutoivumilia rushwa na namna ya kuifikia TAKUKURU kutoa taarifa za vitendo vya rushwa imeendelea katika Mikoa yote kupitia njia za mikutano ya hadhara, vipindi vya redio na runinga inayojazwa upepo viliifikia Mikoa ya Shinyanga, Geita na Simiyu;

(xi) Kituo cha Huduma kwa Mteja kimesaidia kutoa elimu na msaada wa haraka kwa wananchi hususan wanaoombwa rushwa au kucheleweshwa kupatiwa huduma kwa kuwa kinafanya kazi saa ishirini na nne. Wananchi wameweza kuifikia TAKUKURU kwa kupiga simu namba 113, kutuma ujumbe kwenda namba hiyo au kutoa taarifa kwa kupiga *113# yaani mfumo wa USSD *(Unstructured Supplementary Service Data)*. Katika kipindi husika, malalamiko 199,337 yamepokelewa ambapo malalamiko 35,804 yalikuwa kwa njia ya simu, 157,481 kupitia ujumbe mfupi wa simu na 6,052 kupitia USSD;

(xii) Watumishi 214 walipatiwa mafunzo ili kuwajengea uwezo wa kumudu majukumu yao kwa ufanisi. Kati ya hao, watumishi 199 walipata mafunzo ndani ya nchi na watumishi 15 walipata mafunzo nje ya nchi; na

(xiii) Ujenzi wa jengo la makazi ya Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Bahi umekamilika. Jengo hili litatumika kama Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Bahi mpaka hapo jengo la ofisi litakapojengwa.

(c) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

21. *Mheshimiwa Spika,* Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) unaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuwawezesha wananchi wanaomiliki rasilimali na biashara nje ya mfumo rasmi kuwa na uwezo wa kurasimisha mali na hatimaye kushiriki katika uchumi wa soko unaoendeshwa kwa mujibu wa Sheria. Ili kufikia azma hii, MKURABITA inao wajibu wa kuwawezesha Watanzania kutumia mali zao zilizokwisharasimishwa kama dhamana katika kupata mikopo na fursa nyingine katika uchumi wa soko. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Uandaaji wa Hati za Haki Miliki za Kimila 8,790 umefanyika katika Halmashauri za Wilaya 7 za Buhigwe, Uvinza, Mpimbwe, Ikungi, Karagwe, Mkuranga na Nachingwea;

(ii) Ujenzi wa Masjala 2 za Ardhi za Vijiji vya Pwaga na Munguwi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa umekamilika. Aidha, MKURABITA imekamilisha ujenzi wa Masjala 1 ya Ardhi katika Shehia ya Kiungoni, Wilaya ya Wete, Pemba;

(iii) Kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Kituo kimoja cha kurasimisha biashara (one stop centre) kimeanzishwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ambapo huduma muhimu za utoaji wa leseni za biashara, utoaji wa Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN), usajili wa jina la biashara (BRELA), huduma za benki, na Mifuko ya hifadhi ya Jamii zinapatikana sehemu moja. Hadi kufikia Machi, 2017 Kituo kimesajili biashara 3,222 ambapo Shilingi milioni 343 zimekusanywa kutokana na ada za leseni;

(iv) Mafunzo ya kuwajengea uwezo wakulima kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila kukuza mitaji yao yametolewa kwa wakulima 1,068 na Viongozi 219 wa vyama vya wakulima

katika Halmashauri za Wilaya za Mwanga (Vijiji vya Kivulini na Kileo), Meru (Vijiji vya Maweni na Karangai), Mbinga (Vijiji vya Tanga na Tukuzi), Sumbawanga (Kijiji cha Mshani), Kalambo (Kijiji cha Katuka), Korogwe (Vijiji vya Mnyuzi na Kwagunda), Karagwe (Kijiji cha Nyakayanja), na Kilombero (Vijiji vya Idete A na B). Aidha, Mipango Kazi ya Jamii ya Vijiji imetekelezwa kwa kuanzisha vikundi 31 vya uzalishaji, mashamba darasa 4 na SACCOS 3;

(v) Uandaaji wa mwongozo kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Majaribio ya Urasimishaji kwa kutumia dhana ya Mfuko wa Dhamana katika Manispaa ya Iringa na Halmashauri 2 za Mkoa wa Songwe umekamilika;

(vi) Kwa kushirikiana na Ofisi za Taifa za Takwimu Tanzania Bara na Zanzibar, MKURABITA imeandaa Hadidu za Rejea pamoja na Zana za utafiti (Dodoso) ambazo zitatumika kwa ajili ya utafiti na tathmini ya sekta isiyo rasmi nchini. Aidha, MKURABITA imekamilisha uandaaji wa Dhana ya Andiko kwa ajili ya kutafuta fedha za utafiti;

(vii) Kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania, MKURABITA imeshiriki katika uchambuzi wa takwimu na kuandaa ripoti ya matokeo ya utafiti kwa ajili ya utangamano wa dhana za urasimishaji katika Mtaala wa Elimu ya Msingi ambapo washiriki wengi wanaona umuhimu wa kuingiza dhana ya urasimishaji katika Mitaala; na

(viii) MKURABITA iliwasilisha mada katika Vikao vya Kamati za Ushauri za Mikoa ya Singida na Dodoma kwa lengo la kuendelea kutoa elimu ya urasimishaji kwa wadau katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(d) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

22. *Mheshimiwa Spika,* Mfuko wa Maendeleo ya Jamii umeendelea kutekeleza Awamu ya Tatu kwa kuyapa kipaumbele maeneo ya ukuzaji wa uchumi, kuongeza fursa na kupunguza umaskini wa kipato; kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na utawala bora na uwajibikaji.

23. *Mheshimiwa Spika,* katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Jumla ya kaya maskini 1,358,268 zimetambuliwa tangu Mpango wa kunusuru kaya maskini uanze. Kati ya hizo, kaya maskini 1,110,377 zenye jumla ya watu 5,895,230 zimeandikishwa. Kati ya kaya/watu wote waliomo katika Mpango, asilimia 54 ni wanawake. Mpango huu unatekelezwa katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar. Aidha, jumla ya Shilingi bilioni 202.2 zilihawilishwa kama ruzuku kwa kaya maskini;

(ii) Mpango wa kutoa ajira za muda umetekeleza jumla ya miradi 3,553 kutoka katika Vijiji 2,063, Mitaa 329 na Shehia 168 jumla yake ni 2,560 ambapo kaya za walengwa 298,970 zilipata ajira za muda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar. Miradi hiyo ina thamani ya Shilingi bilioni 32. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa malambo ya maji, uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti, uchimbaji wa visima vifupi, uboreshaji wa barabara, uhifadhi wa vyanzo vya maji, na hifadhi ya mazingira. Aidha, jumla ya wawezeshaji 953 wa ngazi ya Halmashauri na 231 kwa upande wa Unguja na Pemba walipewa mafunzo ya uandaaji wa miradi na usimamizi;

(iii) Zoezi la uhakiki wa kaya maskini ambalo ni endelevu lilifanyika na kubaini kuwepo kwa kaya 68,914 nchini kote ambazo zilikosa sifa. Kaya hizi zote zimeondolewa kwenye Mpango. Mgawanyo wa kaya hizo ni kama ifuatavyo:

(a) Kaya zilizokuwa na mwanakaya mmoja ambaye alifariki au wote wamefariki ni 15,833;

(b) Kaya zilizohamia katika Vijiji/Mitaa/Shehia ambapo Mpango haujaanza kutekelezwa ni 8,436;

(c) Kaya ambazo hazikujitokeza mara tatu mfululizo kupokea ruzuku ni 20,914;

(d) Kaya ambazo wananchi walithibitisha kuwa siyo maskini ni 18,919; na

(e) Kaya ambazo baadhi ya wanakaya ni Wajumbe wa Kamati za Usimamizi za Jamii, Halmashauri za Vijiji/Kamati za Mitaa, Viongozi na Watendaji ni 4,812.

(iv) Ukusanyaji wa takwimu za hali halisi ya mahitaji ya miundombinu ya afya, elimu na maji kutoka katika maeneo yote ya utekelezaji 161 ulifanyika na uchambuzi wa takwimu unaendelea ili kutambua mahitaji ya kila eneo la utekelezaji. Jumla ya miradi 72 ya miundombinu ya elimu na afya yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.8 imetekelezwa. Kati ya hiyo, miradi 70 imetekelezwa Tanzania Bara na miradi 2 imetekelezwa Zanzibar (Unguja 1 na Pemba 1). Aidha, mchakato wa kuibua miradi mipya umefanyika ambapo jumla ya Shilingi bilioni 1.9 zimeidhinishwa ili kutekeleza miradi 39 katika Mikoa ya Arusha na Njombe;

(v) Miongozo ya utekelezaji wa shughuli za kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya ilikamilika na kuanza kutumika katika utekelezaji. Miongozo hiyo ilitumika kutoa mafunzo ya stadi za ujasiriamali na mbinu za kuunda vikundi endelevu vya kuweka akiba kwa kaya za walengwa yametolewa kwa wawezeshaji 400 kutoka Halmashauri 18 za Tanzania Bara, Unguja na Pemba. Jumla ya vikundi 5,136 vya kuweka akiba na kuwekeza vyenye wanachama 73,914 viliundwa na jumla ya Shilingi milioni 572 zimetumika;

(vi) Mfumo wa Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa Utambuzi, Uandikishaji, Malipo na Malalamiko ya Walengwa umekamilika na unatumika. katika Ofisi za TASAF zilizoko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 142 za Tanzania Bara pamoja na Unguja na Pemba zimeunganishwa na Makao Makuu ya TASAF kupitia mtandao wa mawasiliano wa TAMISEMI kwa Tanzania Bara na mtandao wa mawasiliano wa Kampuni ya Simu (TTCL) kwa Unguja na Pemba;

(vii) Katika kujenga uwezo wa wadau muhimu katika kutekeleza Mpango kwa ufanisi, mafunzo yalitolewa kwa Wakuu wa Mikoa 29; Makatibu Tawala 25 wa Mikoa; Wakuu wa Wilaya 134; Wakurugenzi 190 wa Halmashauri za Jiji/Manispaa/Miji /Wilaya na Wasaidizi 9 wa Wakuu wa Mikoa. Kwa upande wa Zanzibar, mafunzo yalitolewa kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri 3; Wakuu wa Mikoa 5; Wakurugenzi 31 wa Uratibu; Maafisa Wadhamini 8, Makatibu 7 wa Baraza la Wawakilishi; Wakuu wa Wilaya 11, Wawakilishi 18, Makatibu Tawala 7 na Madiwani 5. Aidha, mafunzo yalitolewa pia kwa wawezeshaji 176,326 kutoka maeneo yote ya utekelezaji; Wajumbe 58,738 wa Kamati za Usimamizi za Jamii; watendaji 4,712 wa Vijiji, Mitaa na Shehia; Wenyeviti 4,490 wa Vijiji, Mitaa na Shehia; walimu 5,174 wa shule za sekondari na msingi; wafanyakazi 2,464 wa afya, wajumbe 16,201 wa Halmashauri za Vijiji, Mitaa na Shehia; na washauri wafuatiliaji, waratibu na wahasibu wa Mpango 340. Pia, mafunzo ya stadi za maisha yametolewa kwa vijana 188 na wanajamii 986;

(viii) Tafiti mbalimbali zenye lengo la kupima ufanisi wa utekelezaji wa Mpango na matokeo yake zimeendelea kufanyika. Tafiti hizo zilihusu Tathmini ya Mpango; tathmini ya Mpango kwa maendeleo ya vijana; na tathmini kuhusu ushiriki na uwezeshwaji wa wanawake. Tafiti hizi ambazo ni za msingi zimekamilika kwa awamu ya kwanza. Awamu ya pili imepangwa kuanza Mwezi Aprili, 2017;

(ix) Mafunzo ya kujenga uelewa pia yamefanyika kwenye Sekretarieti za Mikoa ambapo wajumbe 512 wamejengewa uelewa kwenye Mikoa 26 ya Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu Mpango wa TASAF Awamu ya Tatu; na

(x) Ukaguzi wa ndani ulifanyika ili kuhakikisha endapo fedha zilitumika ipasavyo katika utekelezaji wa Mpango wa TASAF Awamu ya Tatu. Ukaguzi ulifanyika TASAF Makao Makuu pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa 46. Aidha, Wakaguzi wa Nje kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) walifanya ukaguzi wa uhawilishaji fedha kwa walengwa, manunuzi, uendeshaji na thamani ya fedha.

(e) Taasisi ya UONGOZI

24. *Mheshimiwa Spika,* Taasisi ya UONGOZI imeendelea kusimamia malengo yake ya kuwa Kituo cha utaalam wa hali ya juu cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, Watumishi wa Umma na Mahakama.

25. *Mheshimiwa Spika,* katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

(i) Kozi 18 za muda mfupi zimetolewa kwa Viongozi wa Umma 631 ili kuimarisha utendaji wao. Kozi hizi ni kwenye maeneo ya Maadili, Utawala Bora na Uwajibikaji; Mawasiliano Fanisi na Mbinu za Uchambuzi Yakinifu; Mitazamo na Dira; Usimamizi wa Vihatarishi na Udhibiti wa Ndani; Uongozi wa Kimkakati; Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; Ujuzi na Mbinu za Majadiliano ya Mikataba; Usimamizi wa Mipango yenye Matokeo; na Michakato ya Sera;

(ii) Maandalizi ya Programu ya "Stashahada ya Uzamili katika Uongozi" (Post Graduate Diploma in Leadership) yamekamilika. Programu hii inalenga kuwajengea viongozi uwezo wa kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimali watu na rasilimali nyingine na sifa binafsi za kiongozi. Programu hii itatekelezwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto kilichoko Helsinki, Finland. Awamu ya kwanza ya mafunzo/programu inatarajiwa kuanza mwezi huu wa Aprili, 2017 na itahusisha viongozi waandamizi wa Jeshi la Polisi ambapo awamu ya kwanza itahusisha viongozi 32;

(iii) Maandalizi ya Programu ya Mafunzo kuhusu "Majadiliano ya Mikataba ya Kimataifa ya Biashara" yatakayotolewa kikanda yamekamilika. Washiriki watatoka Tanzania, nchi nyingine Barani Afrika na Taasisi za Kikanda, zikiwemo Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Utekelezaji wa Programu hii utaanza mwezi Aprili, 2017;

(iv) Kwa kushirikiana na Taasisi za ndani na nje ya nchi, mikutano 7 ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa ilifanyika kwa lengo la kukutanisha viongozi ili kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu na kuwaongezea uelewa wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu. Jumla ya Viongozi 1,018 walishiriki kutoka Tanzania na nchi mbalimbali ndani na nje ya Afrika. Mikutano ifuatayo ilifanyika:-

(a) Kongamano la Kikanda la Viongozi wa Afrika juu ya "Namna ya Kuendeleza Biashara Barani Afrika" lilifanyika tarehe 28-29 Julai, 2016. Kongamano hili liliandaliwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Mstaafu, Mhe. Benjamin William Mkapa;

(b) Kongamano la Kimataifa kuhusu "Sera zinazohusu Mabadiliko ya Tabia Nchi" lilifanyika tarehe 13-14 Julai,

2016. Kongamano hili liliandaliwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya "Climate Strategies" ya Uingereza;

(c) Kongamano la Kimataifa juu ya namna ya "Kukuza Uwekezaji katika Sekta ya Misitu" liliandaliwa kwa kushirikiana na Serikali ya Finland na Taasisi ya Finn Fund. Kongamano hilo lilifanyika tarehe 15-16 Novemba, 2016;

(d) Kongamano la Kitaifa kuadhimisha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere lilifanyika tarehe 13 Oktoba, 2016. Mada kuu ilikuwa "Mafunzo kwa Viongozi wa Sasa na wa Kizazi cha Baadae". Kongamano hili liliandaliwa kwa kushirikiana na Ubalozi wa China hapa nchini na Taasisi ya Kukuza Urafiki kati ya China na Tanzania;

(e) Kongamano la kitaifa la viongozi juu ya "Nafasi ya Mashirika ya Umma katika Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano" lilifanyika tarehe 28 Februari, 2017. Kongamano hili liliandaliwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina;

(f) Kongamano la Kitaifa kuhusu "Uhuru wa Nchi, Demokrasia na Maendeleo ya Jamii Afrika" lilifanyika tarehe 10 Machi, 2017. Kongamano hili liliandaliwa kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam;

(g) Mkutano wa Kitaifa kujadili "Mikakati ya Tanzania katika kuelekea kwenye Uchumi wa Viwanda" ulifanyika tarehe 31 Machi, 2017. Mkutano huo uliandaliwa kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID).

(v) Vipindi 7 vya mahojiano na viongozi waandamizi na wataalam wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu viliandaliwa na kurushwa kwenye runinga na kuwekwa kwenye tovuti ya Taasisi na mitandao ya kijamii kwa nia ya kuimarisha na

kujenga uwezo wa viongozi wa sasa na wanaochipukia. Vipindi hivi vinaoneshwa na kuonekana Bara zima la Afrika;

(vi) Programu Jumuishi juu ya masuala ya Maendeleo Endelevu imeanzishwa ili kuwezesha utekelezaji wa Malengo ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu. Programu hii inahusisha mafunzo, makongamano, na tafiti juu ya masuala ya maendeleo endelevu;

(vii) Maandalizi ya kuanzisha Programu ya utafiti juu ya "Masuala ya Uongozi Barani Afrika" yamekamilika;

(viii) Utafiti unaohusu "Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)" umekamilika. Utafiti huu ulihusisha miradi 10 ya ubia katika Sekta za Nishati, Miundombinu na Mawasiliano Barani Afrika. Utafiti ulihusisha miradi kutoka Nchi za Tanzania, Nigeria, Ghana, Afrika ya Kusini na Kenya;

(ix) Utafiti kuhusu "Viwezeshi na Vikwazo vya Uongozi Barani Afrika" unaendelea kufanyika kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Birmingham, Uingereza. Utafiti huu unazihusu nchi 5 ambazo ni Tanzania, Uganda, Afrika ya Kusini, Ethiopia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo;

(x) Chapisho kuhusu Maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Mhe. Benjamin Mkapa liko katika hatua za mwisho, na linalohusu Maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili Mhe. Ally Hassan Mwinyi limeanza kuandaliwa. Lengo kuu ni kutoa machapisho (memoirs) kuhusu maisha binafsi na michango ya Marais wastaafu;

(xi) Shindano la insha kwa vijana wa Afrika wenye umri kati ya miaka 18-25 lilifanyika kwa lengo la kuimarisha uwezo wa

kujenga hoja na uelewa katika masuala ya Uongozi. Vijana 532 kutoka nchi 31 za Afrika walishiriki. Kati yao, vijana 111 walitoka Tanzania, sawa na asilimia 21 ya vijana wote walioshiriki. Washindi walikuwa 5, waliotoka Kenya 2, Nigeria 2 na Zimbabwe 1;

(xii) Zoezi kwa vijana wa Afrika kuhusu "Jinsi Teknolojia inavyoweza Kutumika Kuboresha Uwazi, Uwajibikaji na Ufanisi katika Taasisi za Umma" liliandaliwa kwa kushirikiana na Kituo cha Kikanda cha *"Young African Leadership Initiative" (YALI)*. Lengo la zoezi hili ni kuwajengea uwezo wa uchambuzi wa masuala ya kisera na kiutendaji. Zoezi hili lilishirikisha vijana 13 kutoka Tanzania, Kenya, Rwanda, Sudani Kusini, Djibouti, Congo na Ethiopia. Matokeo ya zoezi hili yaliwasilishwa, na vijana husika walipatiwa mrejesho na wataalam;

(xiii) Programu Jumuishi ya Usimamizi wa Rasilimali za Taifa hususan katika Sekta ya Uziduaji (Mafuta, Gesi Asili na Madini) ilitekelezwa kama ifuatavyo:

(a) Mafunzo kwa ajili ya kuijengea uwezo Timu ya Serikali ya Majadiliano ya Mikataba ya Mafuta na Gesi Asili yalitolewa. Kozi 5 zilifanyika kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Columbia, Marekani;

(b) Maandalizi ya Programu ya mafunzo kuhusu "Majadiliano ya Mikataba katika Sekta ya Maliasili" yatakayofanyika kikanda yalikamilika. Programu hii itajikita katika masuala ya majadiliano ya mikataba katika maeneo ya Mabadiliko ya Tabia ya Nchi, Mafuta, Gesi na Madini;

(c) Kongamano la Kikanda kuhusu jinsi ya kuongeza ushiriki wa makampuni ya ndani katika mnyororo wa thamani kwenye Sekta ya Uziduaji liliandaliwa kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na

Mazingira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kongamano hilo lilifanyika tarehe 27-28 Oktoba, 2016 na kuhudhuriwa na viongozi na wataalam 93 kutoka ndani na nje ya Tanzania;

(d) Tafiti 3 zinaendelea kufanyika ambazo ni Athari za Kimazingira katika Sekta ya Uziduaji; Uwekezaji na Matumizi Sawia ya Mapato ya Serikali yatokanayo na Sekta ya Mafuta na Gesi Asili; na Hali ya Sekta ya Uziduaji Nchini kwa mwaka 2016;

(e) Makala 3 juu ya masuala ya uziduaji yaliandaliwa na kuchapishwa kwenye magazeti na tovuti ya Taasisi;

(f) Uratibu na uwezeshaji wa shughuli za Timu ya Serikali ya Majadiliano ya Mikataba ya Mafuta na Gesi unaendelea kufanyika. Timu hiyo kwa sasa inaendelea na majadiliano na Makampuni ya Mafuta ya Kimataifa.

(f) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea

26. *Mheshimiwa Spika,* Mfuko wa Rais wa Kujitegemea umeendelea kutoa mikopo, mafunzo pamoja na ushauri wa kibiashara kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 ni kama ifuatavyo:-

(i) Mikopo 1,425 yenye thamani ya Shilingi milioni 907.30 imetolewa kwa vijana waliohitimu mafunzo katika Vyuo vya Ufundi Stadi vinavyotambuliwa na VETA na SIDO na wanawake wajasiriamali wa Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Njombe na Lindi;

(ii) Walengwa 1,821 wa Mfuko walipata mafunzo ya ujasiriamali, namna ya kujitambua na taratibu za mikopo ya Mfuko;

(iii) Tawi la Lindi limefunguliwa mwezi Novemba, 2016 ambapo Walengwa wa Mfuko 83 walipata mafunzo ya awali na walengwa 46 walipatiwa mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 17.5;

(iv) Kwa kushirikiana na *Plan International*, mafunzo kwa vitendo kuhusu stadi mbalimbali za kazi kama vile ushonaji, utengenezaji wa batiki, n.k yamefanyika kwa vijana 104 wanaoishi katika mazingira magumu katika Mikoa ya Pwani na Morogoro;

(v) Tafiti zilifanyika katika Mikoa ya Lindi na Njombe ambapo zilibaini utayari na uhitaji wa huduma za mikopo kwa kundi lengwa ni mkubwa na hivyo ni fursa nzuri kwa Mfuko kujipanua;

(vi) Maofisa mikopo 10 walipata mafunzo ya utoaji huduma na sera za mikopo; na

(vii) Maofisa 5 kutoka Matawi yote ya Mfuko walipata mafunzo yanayohusu uthibiti na usimamizi wa huduma za mikopo.

OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA WAKALA ZAKE

27. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32) inayojumuisha Wakala zilizo chini yake liliidhinishiwa jumla ya Shilingi 30,341,137,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka. Kati ya fedha hizo, Shilingi 22,791,137,000 ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 7,550,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 kiasi cha Shilingi 18,704,565,589.28 zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizi Shilingi 18,014,565,589.28 zilikuwa kwa ajili ya

Matumizi ya Kawaida na Shilingi 690,000,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

28. *Mheshimiwa Spika,* Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Wakala zake imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora. Aidha, Watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa wananchi pale wanapotoa huduma mbalimbali kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa.

29. *Mheshimiwa Spika,* Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

a) Menejimenti ya Utumishi wa Umma

(i) Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 yamefanyika ili kuiwezesha Serikali kutekeleza Sera ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010 ambayo inalenga kuoanisha na kuwianisha mishahara miongoni na baina ya watumishi wa Taasisi za umma;

(ii) Wizara zimeendelea kujengewa uwezo wa kuandaa Sera pamoja na kufanya tathimini ya utekelezaji wake katika sekta husika ambapo Timu ya Kitaifa ya Wataalam wa Sera inayoratibiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilishirikiana na Wataalamu wa Wizara husika kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Aidha, Rasimu za Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki, Sera ya Taifa ya Serikali Mtandao na Sera ya Taifa ya Mazingira ziliandaliwa kwa mfumo huu;

(iii) Watumishi Housing Company - WHC imetekeleza jukumu la kujenga nyumba zenye gharama nafuu na kuwauzia Watumishi wa Umma kwa utaratibu wa mikopo. Chini ya WHC, Miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba za watumishi inaendelea kutekelezwa katika maeneo ya Bunju

(Mabwepande), Kigamboni (Gezaulole) na Watumishi Magomeni Flats (Dar es Salaam), Kisesa (Mwanza), na Mizani Mkundi (Morogoro). Aidha, Kampuni inaendelea na maandalizi ya kujenga nyumba katika maeneo mbalimbali nchini; ambayo ni, Mailimoja Setelite City (Kibaha, Pwani), Njedengwa (Dodoma), Mangamba (Mtwara), Tunduma-Mpemba (Mbeya), Pongwe City (Tanga), Shinyanga (Shinyanga), Usa River (Arusha), na Mtwelo Beach (Lindi);

(iv) Vibali vya ajira mpya kwa nafasi 9,721 vimetolewa kwa waajiri ikijumuisha nafasi 3,174 kwa Jeshi la Polisi, 1,000 kwa Jeshi la Magereza, 852 kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, nafasi 297 kwa Jeshi la Uhamiaji pamoja na nafasi 50 kwa ajili ya ajira za wataalamu wa Afya katika Hospitali ya Mloganzila. Aidha, kibali cha ajira kwa nafasi 4,129 za walimu wa Masomo ya Sayansi na Hisabati pamoja na nafasi 219 kwa ajili ya kuajiri Mafundi Sanifu wa Maabara za shule vilitolewa na taratibu za ajira kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI;

(v) Uhakiki wa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 18,823 yenye thamani ya Shilingi 32,859,479,490.37 umefanyika na kuyaingiza kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mshahara kwa ajili ya malipo. Aidha, madai ya malimbikizo ya Mshahara ya Watumishi 12,973 yenye jumla ya Shilingi 21,615,565,432.71 bado yanaendelea kuhakikiwa;

(vi) Watumishi 19,708 wameondolewa kwenye Orodha ya Malipo ya Mshahara ya Watumishi wa Umma (Payroll) kutokana na kustaafu, kuacha kazi, kufariki, kufukuzwa kazi na kumalizika kwa mikataba kwa lengo la kudhibiti watumishi hewa na mishahara batili;

(vii) Kufanya ukaguzi na uhakiki wa matumizi ya Rasilimaliwatu miongoni mwa waajiri katika Mikoa yote Tanzania Bara kwa lengo la kuongeza uwajibikaji katika kusimamia rasilimaliwatu kwenye Taasisi za Umma;

(viii) Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili umefanyika katika Taasisi za Umma 30. Aidha, Ufuatiliaji umeonesha jumla ya makosa 313 kati ya 371 yaliyohusiana na ukiukwaji wa Maadili katika Taasisi hizo yalishughulikiwa. Hii ni sawa na 84%. Kiwango cha jumla (overall annual score) cha ufuatiliaji kwa Mwaka wa fedha wa 2016/17 kitatolewa baada ya kufanyika kwa ufuatiliaji wa mwisho wa mwaka wa fedha 2016/17;

(ix) Mafunzo ya maadili ya utendaji katika Utumishi wa Umma yametolewa kwa Watumishi 9,763 kutoka katika Taasisi 20 za Umma. Aidha, viapo vya Ahadi ya Uadilifu kwa Watumishi wa Umma 165,481 kutoka katika Taasisi za Umma 172 vimeratibiwa;

(x) Elimu kuhusu Maadili ya Watumishi wa Umma imetolewa, ambapo jumla ya makala 2 zilitolewa na vipindi 2 vya Runinga vilirushwa kama sehemu ya maadhimisho ya Kitaifa ya Wiki ya Uadilifu na Haki za Binadamu yaliyofanyika mwezi Disemba, 2016;

(xi) Ofisi imeendelea kusimamia na kuratibu mafunzo ya Watumishi wa Umma katika ngazi mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Watumishi wa Umma 654 walihudhuria mafunzo mbalimbali nje ya nchi kupitia ufadhili wa Serikali kama ifuatavyo:- India (302), Japan (91), China (44) Jamhuri ya Korea Kusini (66), Australia (36), Uholanzi (106) na Misri (9);

(xii) Taasisi za Umma zimeendelea kuwezeshwa kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu na Mipango ya Urithishanaji Madaraka. Lengo ni kuziwezesha Taasisi hizo kutambua mahitaji ya sasa na ya baadae ya Rasilimaliwatu ili kuyatumia vizuri katika kutekeleza Mipango Mkakati yake. Taasisi zilizowezeshwa ni Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Chuo Kikuu cha Sayansi, na Teknolojia Mbeya (MUST), na Sekretarieti za

Mikoa ya Geita, Shinyanga na Mbeya pamoja na Mamlaka zao za Serikali za Mitaa;

(xiii) Taasisi za Umma 4 zimewezeshwa kuhuisha Mipango yao ya Mafunzo. Taasisi zilizowezeshwa ni:- Chuo cha Utalii, Wakala ya Serikali Mtandao (eGA), Bodi ya Wataalam wa Ununuzi (PSPTB), na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini Tanzania (RITA).

(xiv) Usanifu wa Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma umeanza kufanyika kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Uingereza (DFID) na Benki ya Dunia. Usanifu wa Programu ya Maboresho umeanza kwa kufanya uchambuzi wa vikwazo vya utendaji kazi vya Kitaasisi na Uchambuzi wa hali ya kiuchumi na kisiasa;

(xv) Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Ofisi/Wizara 20 na Taasisi za Umma 3 imehuishwa ili kuendana na mahitaji ya sasa kwa nia ya kupunguza ukubwa wa Serikali na kuimarisha utoaji wa huduma na uwajibikaji kama ilivyo dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano;

(xvi) Uandaaji wa Nyaraka za kuanzisha Wakala ya Barabara za Serikali za Mitaa (Tanzania Rural and Urban Agency (TARURA) umekamilika na Nyaraka hizo zimepelekwa kwenye Mamlaka za Serikali (Katibu Mkuu Kiongozi) kwa ajili ya kuidhinishwa;

(xvii) Kanzidata ya Fomu zinazotumika kwenye Taasisi za Serikali imeanzishwa na mpaka sasa fomu 409 kutoka Taasisi 18 zimeshawekwa kwenye Mfumo. Ufuatiliaji kwa Taasisi zingine unaendelea;

(xviii) Mifumo mitano ilifuatiliwa kwenye Wakala za Serikali 35 na matokeo yanaonesha utekelezaji wake umeimarika. Mifumo hiyo ni: Mpango Mkakati, Mfumo wa Malalamiko, Mfumo wa

Wazi wa Upimaji wa Utendaji Kazi (OPRAS), Mkataba wa Huduma kwa Mteja; na Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji;

(xix) Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango Mkakati, Bajeti na Utoaji Taarifa umehuishwa kwa kushirikisha wadau wakuu kwenye uandaaji wa mipango na bajeti serikalini. Ikijumuisha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu);

(xx) Ofisi kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Marekani kupitia Mradi wa PS3 ilifuatilia utekelezaji wa Mifumo ya Utendaji kazi kwa majaribio kwenye Mikoa 2 (Dodoma – Halmashauri ya Bahi na Chemba na Iringa – Halmashauri ya Iringa Vijijini na Kilolo);

(xxi) Elimu juu ya Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji kwa Wizara 12, Mikoa 25 na Halmashauri zote zilizo chini ya Mikoa hiyo ilitolewa kwa njia ya mtandao (video conference). Elimu hiyo ilitolewa katika vikao 3 ambapo washiriki 566 walifikiwa kwa gharama nafuu ikilinganishwa na gharama ambayo ingetumika endapo watumishi hao wangesafiri kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya mafunzo hayo.

(xxii) Ukusanyaji na uhuishaji wa takwimu za watumishi wenye ulemavu katika Utumishi wa Umma na kuzitunza takwimu hizo kwa maamuzi na matumizi mbalimbali ya Serikali umefanyika. Aidha, ufuatiliaji wa utekelezaji wa mwongozo wa VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza katika Taasisi za Umma umefanyika;

(xxiii) Uratibu wa uhamisho na uteuzi katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia taarifa za kiutumishi, umeendelea kufanyika ambapo vibali 2,044 vya Uhamisho, 1,563 vya kuazimwa watumishi na 189 vya likizo bila malipo vilitolewa. Katika kipindi hiki Watumishi 306 wameteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali za Uongozi;

(xxiv) Jumla ya malalamiko 1,346 kati ya 1,384 sawa na asilimia 97 yanayohusu ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma yameshughulikiwa;

(xxv) Huduma za Kawaida kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa (Wastaafu 11 na wajane 5 zimeendelea kutolewa;

(xxvi) Uratibu wa utekelezaji wa eneo la Serikali Mtandao chini ya Programu ya Miundombinu ya Mawasiliano ya Kikanda, kwa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika (RCIP) umeendelea kufanyika ambapo miradi inayotekelezwa katika Programu hiyo ipo katika hatua mbalimbali. Miradi hiyo ni Mfumo wa Taarifa za Usajili wa Vizazi na Vifo (Birth and Death Registration system); Mfumo wa Taarifa za Biashara (National Business Portal); Mfumo wa Taarifa za Kitabibu (Telemedicine); Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali (Government Network); Mfumo wa Kielekroniki wa Nyaraka (e-Records Management and Preservations); na Mfumo wa Taarifa za Ununuzi kwa Njia ya Kielektroniki (e-Procurement);

(xxvii) Uainishaji wa mahitaji ya miundombinu katika Idara za Afya, Elimu, Mifugo na Kilimo katika Sekretariati za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) umekamilika na mfumo huo umeboreshwa kufuatana na mahitaji hayo na taratibu za usimamizi wa masuala ya rasilimaliwatu katika Idara hizo. Ufungaji wa Mfumo katika Idara hizo unaendelea kufuatia mafunzo kwa watumiaji wa mfumo kukamilika;

(xxviii) Mafunzo kwa Maafisa Elimu na Makatibu Afya 633 na Maafisa TEHAMA 116 kutoka Idara za Elimu, Afya na Kitengo cha TEHAMA katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa yamekamilika na walengwa wameanza kutumia mfumo huo. Hadi sasa, jumla ya Taarifa za Shule za Msingi 6,400, Shule za Sekondari 1,730 na Vituo vya Afya/Zahanati/Hospitali 1,881 zimeshaingizwa kwenye mfumo;

(xxix) Rasimu ya mwisho ya Sera ya Serikali Mtandao imekamilika na inaandaliwa kuwasilishwa kwenye mamlaka za maamuzi Serikalini.

b) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)

30. *Mheshimiwa Spika,* Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala; kutoa shauri za kitaalam kufanya utafiti na machapisho mbalimbali ya kitaalam katika Utumishi wa Umma.

31. *Mheshimiwa Spika,* katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:

(i) Mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma yalifanyika kwa Watumishi 476;

(ii) Mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa Watumishi wa Umma, ambapo watumishi 594 walinufaika na mafunzo ya awali na watumishi 968 walipata mafunzo ya muda mfupi na wengine 13,990 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Cheti, na Stashahada katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili, Kompyuta, Utunzaji wa Fedha za Umma, na Menejimenti ya Rasilimali Watu, Usimamizi wa Manunuzi ya Umma, Uongozi na Utawala Bora;

(iii) Maandiko 5 ya ushauri wa kitaalamu yameandaliwa. Aidha, kazi ya kutoa ushauri kwenye eneo 1 la kitaalamu imefanyika;

(iv) Toleo la kwanza la Jarida la Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC Journal) lipo katika hatua ya uchapishaji. Aidha, makala 5 za kitaalam katika Utumishi wa Umma zimechapishwa katika majarida mbalimbali ndani na nje ya nchi;

(v) Mafunzo kwa Watumishi wa Chuo cha Utumishi wa Umma yamedhaminiwa kama ifuatavyo: 11 Shahada ya uzamivu; 10 Shahada ya uzamili, 9 Shahada ya kwanza, 2 Stashahada na watumishi wengine 70 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi, katika maeneo yafuatayo: Kuongeza stadi za kuandika ripoti za kitafiti; Udhibiti wa maambukizi ya VVU na UKIMWI mahali pa kazi pamoja na Magonjwa Sugu Yasiyoambulizwa;

(vi) Uhakiki wa wakazi wanaostahili kulipwa fidia kwenye eneo linalotarajiwa kujengwa Chuo cha Utumishi wa Umma Wilayani Rufiji unaendelea chini ya usimamizi wa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Rufiji;

(vii) Chuo kinashirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida kukamilisha Mpango Kabambe (Master plan) ya eneo la Chuo la ekari 89; na

(viii) Kukamilisha malipo na umilikishwaji wa eneo la Chuo katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

c) Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA)

32. *Mheshimiwa Spika,* Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao imeendelea kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo maalum ya muda mfupi kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

33. *Mheshimiwa Spika,* katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zimetekelezwa:

(i) Mafunzo yametolewa kwa jumla ya washiriki 1,368 ambapo kati ya hao wanaume ni 842 na wanawake ni 526, katika maeneo ya Uongozi, Utawala Bora, Maadili, Anuai za jamii, TEHAMA na stadi za kuboresha utendaji kazi. Watumishi wa umma walikuwa ni asilimia 92 ya washiriki wote;

(ii) Wakala kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi kwa kutumia Teknolojia ikiwemo Chuo cha Serikali cha Kenya, Chuo cha Menejimenti cha Uganda na "UNESCO Institute of Life Long Learning" kilichopo Hamburg – Ujerumani imepanua wigo wa kutoa mafunzo katika maeneo ya Uongozi na Menejimenti, ambapo watumishi wa umma watapata fursa za mafunzo kutoka kwa wataalam wa nje ya nchi bila ya kusafiri na kwa gharama nafuu;

(iii) Wakala imekamilisha ufungaji wa vifaa vya Mtandao na mawasiliano kwa njia ya video katika Ofisi yake ya Arusha;

(iv) Kuongeza ubora wa huduma kwa wateja kwa kuweka kompyuta za kisasa 10 kwenye maabara ya kompyuta ya Wakala;

(v) Watumishi 6 wa Wakala wamejengewa uwezo kwa kupewa mafunzo ya muda mfupi na wa kati;

(vi) Huduma ya mawasiliano kwa njia ya video imeendelea kutumika na Mahakama katika kuleta mashahidi. Aidha, Madaktari 88 kutoka Taasisi mbalimbali nchini, waliunganishwa na madaktari bingwa kutoka nchi 13 za Afrika, Amerika na Asia na kujadili changamoto za tiba ya malaria na uboreshaji wa tiba za mifupa; na

(vii) Wakala imefanya majaribio ya teknolojia ya mawasiliano kwa njia ya video inayotegemewa kutumia masafa ya intaneti "bandwidth" kidogo hivyo kuwezesha mawasiliano hata sehemu zenye upungufu wa masafa ya intaneti.

d) Wakala ya Serikali Mtandao (eGA)

34. *Mheshimiwa Spika,* Wakala ya Serikali Mtandao imeendelea kutekeleza Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ya Mwaka 2016 katika Utumishi wa Umma ili kuongeza ufanisi, kupunguza gharama na kuimarisha uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, Wakala

ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kukuza matumizi ya TEHAMA serikalini kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wananchi kwa usalama, urahisi na kwa gharama nafuu.

35. *Mheshimiwa Spika,* katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Wakala imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Awamu ya kwanza ya ujenzi wa vituo vikuu vya kuhifadhi taarifa na mifumo ya Serikali (Government Data Centre) imekamilika na vituo vimeanza kutumika. Lengo la vituo hivi ni kuongeza na kuimarisha usalama wa mifumo na taarifa za Serikali na kuongeza uhakika wa upatikanaji wa taarifa katika kutekeleza majukumu ya kila siku;

(ii) Jumla ya Taasisi 63 za Serikali zimeunganishwa katika Mfumo wa Mawasiliano kwa Njia ya Barua pepe (Government Mailing System - GMS) na hivyo kufanya Taasisi zilizounganishwa kutumia mfumo huo kufikia 201. Mfumo huu umeimarisha mawasiliano kwa njia ya barua pepe na kuongeza usalama wa kubadilishana taarifa;

(iii) Jumla ya Taasisi 72 zimeunganishwa kwenye Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Government Network) kwa lengo la kuziunganisha Taasisi za Serikali katika mtandao mmoja wa mawasiliano ya kielektroniki (taarifa, sauti na video) ili kuboresha usalama wa taarifa na kupunguza gharama za mawasiliano. Uunganishaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 77 umekamilishwa kwa asilimia 50. Aidha, Uunganishaji wa mtandao kwa 'fiber' kwenye mikoa 20 ili kuiunga na Mkongo wa Taifa kwa dhumuni la kurahisisha uunganishwaji wa mikoa hii kwenye mtandao wa mawasiliano serikalini umeendelea;

(iv) Kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali, mifumo mbalimbali ya TEHAMA imetengenezwa ikiwa ni pamoja na:-

a) Mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia utekelezaji wa ahadi na maagizo ya viongozi wakuu wa nchi, na Ilani ya Chama Tawala;
b) Mfumo wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kufuatilia utekelezaji wa mipango kazi (Utumishi Dashboard);
c) Mfumo wa Vibali vya Kusafiri Nje ya Nchi (Travel Permit System),
d) Mfumo Mkuu wa Kusimamia Malipo na Maduhuli ya Serikali Kielektroniki (Government Payment Gateway);
e) Mfumo unaotumiwa na wananchi kutoa taarifa za matukio ya rushwa kwa TAKUKURU kwa kutumia simu za mikononi na namba maalum (113 na *113# );
f) Mfumo wa kuiwezesha Tume ya Utumishi wa Umma kutekeleza majukumu yake;
g) Mfumo wa Usimamizi na Uratibu wa Majengo ya Serikali unaotumiwa na Wakala wa Majengo (TBA);
h) Kuboresha Mfumo wa Kuhifadhi Taarifa za Bunge (POLIS); na
i) Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali na Miradi ya TEHAMA Serikalini.

(v) Mfumo wa Kutoa Huduma kwa Njia ya Simu za Mkononi (Government Mobile Platform) umeboreshwa kwa kutengeneza miundo mbinu ya kutoa huduma ya Ujumbe Mfupi (SMS Gateway) na kwa Menyu (USSD Gateway) kupitia namba maalum *152*00# ambapo mpaka sasa jumla ya Taasisi 28 za Serikali zinatumia huduma hii; Mfumo huu umezirahisishia taasisi za Serikali kuweza kujenga mfumo wa kutolea huduma kwa njia ya simu za mikononi kwa muda mfupi ukilinganisha na ilivyokuwa hapo awali. (Kwa mfano mfumo uliokuwa unajengwa kwa miezi mitatu unaweza kujengwa ndani ya siku saba kukamilika;

(vi) Mafunzo kwenye masuala ya Serikali Mtandao yametolewa kwa watumishi wa Taasisi 90 za Serikali ili kujenga uwezo

wao wa kubuni, kujenga na kusimamia miundombinu na mifumo mbalimbali inayotumiwa na Taasisi husika;

(vii) Mfumo wa Kielekroniki wa Masjala (e-Office) umetengenezwa ili kurahisisha ubadilishanaji wa nyaraka na utoaji wa maamuzi Serikalini. Mfumo huu unatumiwa na Taasisi 6 za Serikali katika awamu ya majaribio. Taasisi hizo ni Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Wakala ya Serikali Mtandao, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma;

(viii) Mfumo/Dawati la Kielektroni la Huduma kwa Wateja umeboreshwa kuimarisha utoaji wa msaada wa kiufundi kwa wataalam wa TEHAMA wa Taasisi za Serikali. Hadi sasa, jumla ya Taasisi 154 zinatumia Mfumo huu unaopatikana kupitia http://helpdesk.ega.go.tz, egov.helpdesk@ega.go.tz na simu namba 0764 292 299;

(ix) Usimamizi wa Viwango, Miongozo na Taratibu za Serikali Mtandao ulitekelezwa kwa kuthibitisha miradi/mifumo mbalimbali ya TEHAMA pamoja na kukagua mifumo mbalimbali ya Taasisi 12 za Serikali;

(x) Elimu kwa Umma kuhusu matumizi ya TEHAMA imetolewa kwa kuzalisha na kurusha vipindi vya runinga kupitia Televisheni ya Taifa na Tovuti ya Wakala. Jumla ya vipindi 52 vinaandaliwa ambapo vipindi vitatu vimesharushwa.

## SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

36. *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa Shilingi 6,441,908,200. Kati ya fedha hizo Shilingi 5,441,708,200 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 1,000,000,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2017 Shilingi 3,292,716,100 za Matumizi ya Kawaida kilipokelewa na kutumika.

Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, Shilingi 123,441,000 zilipokelewa na kutumika.

37. *Mheshimiwa Spika,* katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Malalamiko 186 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 130 yalihusu Sheria ya Maadili ya Viongozi na malalamiko 56 hayakuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Malalamiko hayo yanajumuisha maeneo ya migogoro ya ardhí, rushwa, jinai, nk. Uchunguzi wa awali umefanyika kwa malalamiko 9 yanayohusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Malalamiko 121 yaliyosalia yapo katika hatua mbalimbali za kiuchunguzi. Aidha, malalamiko 56 ambayo hayakuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, walalamikaji walipewa ushauri na mengine yalielekezwa kwenye mamlaka zinazohusika;

(ii) Viongozi wa Umma 15,881 walitumiwa Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Disemba, 2016. Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya Viongozi wa Umma 15,346 ambao ni sawa na asilimia 97.3 wamerejesha Fomu hizo. Viongozi walioshindwa kurejesha Matamko yao kwa wakati wamekumbushwa kufanya hivyo na watakaoshindwa kutoa sababu za msingi za kutorejesha kwa wakati watafikishwa katika Baraza la Maadili;

(iii) Viongozi 116 kati ya 500 kwa mwaka wa fedha 2016/17 walihakikiwa. Aidha, Viongozi 384 waliosalia watahakikiwa katika kipindi cha Aprili-Juni, 2017. Viongozi walioonekana kuwa na tofauti au kasoro katika matamko yao wametakiwa kutoa maelezo ya kasoro au tofauti hizo na wale ambao hawatakuwa na maelezo yanayoridhisha watafikishwa kwenye Baraza la Maadili kwa uchunguzi wa kina;

(iv) Viongozi 15,524 walisaini Hati ya Ahadi ya Uadilifu na wale ambao hawajasaini wanaendelea kupewa elimu ya umuhimu wa kusaini hati hiyo. Sekretarieti imekuwa ikitoa elimu mara kwa mara hasa pale viongozi wa kitaifa wanapoapishwa kuingia katika madaraka;

(v) Elimu ilitolewa kwa Viongozi wa Taasisi za Umma 1,056, pamoja na Watumishi wa Umma na wananchi 2,718 kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, Klabu 7 za Maadili zilianzishwa katika Shule za Msingi;

(vi) Siku ya Maadili Kitaifa iliadhimishwa tarehe 10 Disemba, 2016 kwa kushirikiana na Taasisi za Serikali zinazosimamia masuala ya utawala bora, uwajibikaji, haki za binadamu, mapambano dhidi ya rushwa na maadili. Aidha, elimu kwa viongozi wa Taasisi za Umma na wananchi wapatao 680 ilitolewa kupitia Wiki ya Huduma kwa Wateja (Viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es Salaam), matembezi ya watumishi, midahalo 2 inayohusu maadili na kupitia vipindi vya redio, luninga na makala katika magazeti mbalimbali katika kuadhimisha siku hiyo;

(vii) Sekretarieti imeimarisha uwezo ambapo watumishi 80 walipatiwa mafunzo ya juu yaliyofanyika katika Chuo cha Maafisa wa Polisi, Kidatu Morogoro. Mafunzo hayo yalijumuisha namna bora ya kuhakiki mali na madeni ya viongozi wa umma, kufanya uchunguzi, uendeshaji wa kesi katika Baraza la Maadili, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, utakatishaji wa fedha haramu na Mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Taarifa za Kimaadili;

(viii) Ujenzi wa Jengo la Ofisi za Maadili Kanda ya Kusini lililopo Mtwara ulikamilika mwezi Agosti, 2016 na Ofisi ilizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan mwezi Septemba, 2016;

(ix) Uzinduzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Taarifa za Kimaadili ulifanyika tarehe 10 Machi, 2017. Mfumo huu

utawezesha na kufanikisha kukusanya, kuchakata, kutunza taarifa na kumbukumbu mbalimbali kutoka kwa Viongozi wa Umma kuhusu mali na madeni waliyonayo wao binafsi, familia zao, kwa kila mwaka na taarifa kuhusu malalamiko ya ukiukwaji wa maadili unaofanywa na Viongozi wa Umma dhidi ya wananchi. Taarifa na kumbukumbu hizo huchambuliwa na pale inapobidi hufanyika uhakiki unaoiwezesha Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuchukua hatua stahiki dhidi ya Viongozi wasiokuwa waadilifu kama njia mojawapo ya kujenga na kuimarisha Utawala Bora na Uwajibikaji Serikalini na Taifa kwa ujumla;

(x) Maandalizi ya ujenzi wa Ofisi za Maadili Dodoma yameanza; na

(xi) Utafiti kuhusu hali ya Maadili ya Viongozi wa Umma ulifanyika. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa yapo malalamiko ya matumizi mabaya ya madaraka kwa Viongozi wa Umma kwa asilimia 39 na matumizi mabaya ya mali za umma kwa asilimia 20. Aidha, asilimia 70 ya waliohojiwa wana uelewa kuhusu masuala ya Mgongano wa Maslahi. Kwa ujumla utafiti unaonesha kuwa hali ya maadili kwa Viongozi wa Umma ni nzuri ingawa zipo changamoto kadhaa ambazo ni lazima zifanyiwe kazi. Utafiti huo ulihusisha makundi mbalimbali wakiwemo Viongozi wa Umma 573, wananchi 1,625, makampuni binafsi 62 na AZAKI 50 na ulifanywa kwa ushirikiano kati ya Mshauri Mwelekezi na wataalam kutoka Sekretarieti ya Maadili. Utafiti ulifanyika katika Mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Mtwara, Arusha, Iringa, Mwanza, Singida na Shinyanga.

## SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

38. *Mheshimiwa Spika,* Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imeendelea kutafuta wataalam wenye ujuzi na kuandaa mfumo wa Kanzidata za Wataalam hao ili kurahisisha utaratibu wa ajira; kuandaa orodha ya wahitimu wa vyuo vikuu na wataalam

wenye weledi kwa madhumuni ya kurahisisha rejea na ujazaji wa nafasi wazi za ajira katika Utumishi wa Umma; kutangaza nafasi wazi za kazi zinazotokea katika Utumishi wa Umma na kufanya usaili na kuwashauri waajiri kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na mchakato wa ajira.

39. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iliidhinishiwa Jumla ya Shilingi 2,205,404,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, Jumla ya Shilingi 2,121,650,583 zilikuwa zimepokelewa na kutumika.

40. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Sekretarieti imehakiki vyeti vya waombaji kazi 39,511 ambapo kati ya hivyo vyeti 1,951 vilibainika kuwa ni vya kughushi na wahusika waliondolewa katika mchakato pamoja na vyeti hivyo kuchukuliwa na kuwasilishwa kwa mamlaka husika kwa ajili ya hatua zaidi;

(ii) Sekretarieti ilisimamia na kuendesha mchakato wa ajira ya watendaji wakuu wa Taasisi za Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini na nafasi 1 ya Benki ya Azania. Aidha, ilishiriki pia kwa kutoa utaalamu katika kuendesha mchakato wa usaili wa nafasi 3 za Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, nafasi 1 ya Wakala wa Umeme Vijijini na nafasi 1 ya Shirika la Posta Tanzania;

(iii) Sekretarieti imeanza kutengeneza kanzidata ya Maafisa Waandamizi na wenye taaluma/ujuzi maalum ili kurahisisha mchakato wa kujaza nafasi wazi za juu katika Utumishi wa Umma endapo Serikali itahitaji. Hadi kufikia Februari 2017 taarifa za Maafisa Waandamizi 1,840 zimepokelewa kutoka Wizara 5, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya 45, Wakala 4, vyuo Vikuu 3 na Taasisi 14;

(iv) Umefanyika utafiti uliohusisha mahojiano kwenye jumla ya Taasisi 18 katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kupata mrejesho wa utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa michakato ya ajira pamoja na utendaji wa Sekretarieti. Taasisi zilizohusika ni Wizara 5, Ofisi za Wakuu wa Mikoa 2, Wakala wa Serikali 4, Idara Zinazojitegemea 2, Manispaa 3 na Halmashauri 2;

(v) Sekretarieti imekamilisha maandalizi ya kuunganisha mfumo wa maombi ya kazi na ule wa kutunza taarifa za wananchi unaomilikiwa na Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa ili kuhakiki kuwa wanaoajiriwa wanakuwa na sifa stahiki;

(vi) Sekretarieti imefungua ofisi Zanzibar kwa ajili ya kurahisisha mchakato wa ajira katika taasisi za Muungano. Watumishi 3 wamehamishiwa katika ofisi hiyo ambayo tayari imewekewa samani na vitendea kazi;

(vii) Kwa kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao, uboreshaji na uimarishaji unaendelea kwenye mfumo wa kielektroniki wa kuendesha mchakato wa ajira na utunzaji kumbukumbu za wasailiwa na wataalam mbalimbali;

(viii) Sekretarieti imeendelea kuwahudumia wananchi wanaohitaji msaada wa namna ya kutumia mfumo wa maombi ya kazi kwa njia ya kielektroniki (Recruitment Portal) ana kwa ana, barua pepe na kwa njia ya simu; na

(ix) Sekretarieti ya Ajira imewezesha watumishi 4 kupata mafunzo ya muda mrefu nchini na watumishi 4 mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi.

TUME YA UTUMISHI WA UMMA

41. *Mheshimiwa Spika,* Tume ya Utumishi wa Umma imeendelea kuhakikisha kuwa masuala ya Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma yanaendeshwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo zinatumika vizuri kwa lengo la kuimarisha utendaji unaozingatia malengo na matokeo yanayopimika. Aidha, Tume ni Mamlaka ya Rufaa kwa Watumishi wa Umma dhidi ya maamuzi yanayotolewa na mamlaka zao za nidhamu.

42. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha wa 2016/17 Tume ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kiasi cha Shilingi 3,717,876,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2017 kiasi cha Shilingi 3,738,193,089 zilikuwa zimetolewa na kutumika.

43. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Tume ya Utumishi wa Umma ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Rufaa 75 ziliamuliwa ambapo 14 zilikubaliwa, 49 zilikataliwa na 12 zilitupiliwa mbali kwa kuwa zilikatwa nje ya muda;

(ii) Malalamiko 47 ya Watumishi wa Umma yalitolewa uamuzi;

(iii) Ukaguzi wa kawaida wa rasilimali watu umefanyika katika Taasisi 41 ambazo ni Idara Zinazojitegemea 2, Sekretarieti za Mikoa 5, Wakala 3, Taasisi ya Umma 1 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 30;

(iv) Ukaguzi Maalum ulifanyika katika Manispaa ya Kinondoni;

(v) Wadau wa Tume walielimishwa kuhusu taratibu za rufaa katika Utumishi wa Umma na taratibu za kuwachukulia hatua za nidhamu Watumishi wa Umma kupitia utoaji wa makala 1, tovuti 1 ya Tume na mikutano 3 na waandishi wa habari na kupitia wiki ya maadili;

(vi) Watumishi 69 wa Tume walielimishwa kuhusu VVU na UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa na mapambano dhidi ya rushwa. Aidha, huduma kwa watumishi wa Tume wanaoishi na VVU na UKIMWI zilitolewa;

(vii) Watumishi 19 wa Tume waliwezeshwa kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya kuongeza ujuzi katika masuala ya rasilimali watu, na utunzaji wa kumbukumbu.

BODI YA MISHAHARA NA MASLAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

44. *Mheshimiwa Spika,* Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma imeendelea kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mishahara na kupendekeza kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya viwango vya mishahara, posho na mafao katika Utumishi wa Umma kwa ujumla. Vile vile, Bodi ina wajibu wa kumshauri Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya misingi ya miundo ya mishahara katika Utumishi wa Umma.

45. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Bodi ya Mishahara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 1,859,845,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 jumla ya Shilingi 926,501,520 zilipokelewa na kutumika.

46. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha wa 2016/17 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

(i) Rasimu ya Tathmini ya Kazi inayolenga kuhuisha miundo ya mishahara ya Watumishi wa Umma imepitiwa na wataalam kutoka kwenye Wizara na Taasisi mbalimbali wanaounda Kamati ya Tathmini ya Kazi na kurejeshwa kwa Mtaalam Mwelekezi kwa ajili ya marekebisho ya mwisho; na

(ii) Bodi imefanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Bodi wa mwaka 2013/14 hadi 2017/18 na kuandaa Mpango Mkakati wa mwaka 2016/17 hadi 2020/21.

UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI (PDB)

47. *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Bunge liliidhinisha Shilingi 27,616,107,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, Shilingi 397,278,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 27,218,829,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2017 Shilingi 3,499,096,330 fedha za Miradi ya Maendeleo zilipokelewa na kutumika.

48. *Mheshimiwa Spika,* katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Kuwezesha upimaji wa udongo na uandaaji wa ramani za matumizi ya udongo katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini (SAGGOT Regions) kupitia Mradi wa *Tanzania Soil Information Service (TanSIS)* ulio chini ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na Taasisi zake za utafiti. Ukusanyaji wa sampuli za udongo umefanyika na kazi ya uchunguzi inaendelea. Aidha, ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mradi unafanyika ili kuhakikisha matokeo yanapatikana kwa wakati;

(ii) Kuliwezesha Jeshi la Polisi katika Mpango wa Usalama wa Raia na Mali Zao kwa kufanya tathmini ya utayari katika Mikoa ya Kipolisi ya Ilala, Temeke, Mwanza, Arusha, Dodoma na Geita. Tathmini hiyo imefanyika mwezi Septemba, 2016 hadi Februari, 2017;

(iii) Kuratibu zoezi la upembuzi yakinifu wa takwimu za Sekta ya Kilimo uliosaidia zoezi la kumalizia uandaaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Sekta ya Kilimo (ASDP II);

(iv) Kwa kushirikiana na Mahakama, Kikosi kazi cha Mahakama kimejengewa uwezo wa kusimamia vipaumbele kwa kutumia mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN);

(v) Kuliwezesha Jeshi la Polisi kuhamasisha wadau katika kusaidia Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni kujenga vituo vidogo vya polisi 3 vya muda katika matukio mengi ya uhalifu ya Manzese, Coco Beach na Masaki. Aidha, uwezeshaji wadau pia umefanyika katika ujenzi wa Kituo cha Polisi Madale pamoja na hanga la makazi la Kikosi cha Kuzuia Fujo (FFU) Kunduchi; na

(vi) Kuliwezesha Jeshi la Polisi kuhamasisha wadau katika kusaidia ujenzi wa Kituo cha kisasa cha mawasiliano katika Kituo cha Polisi cha Kati Dar es salaam ambacho kimefungwa vifaa vya kufuatilia mwenendo na matumizi ya magari ya doria. Kituo hicho kilizinduliwa Mwezi Julai, 2016.

## IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

49. *Mheshimiwa Spika,* Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa imeendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za utunzaji kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za Umma kwa mujibu wa Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na. 3 ya Mwaka 2002. Aidha, Idara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya Mwaka 2004 katika kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu (Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume).

50. *Mheshimiwa Spika,* Katika mwaka wa fedha 2016/17, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 1,293,851,000.

51. *Mheshimiwa Spika,* Hadi kufikia Machi, 2017 Shilingi 990,762,300 zilipokelewa na kutumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

52. *Mheshimiwa Spika,* Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Idara ya Kumbukumbu imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Uwekaji wa Mfumo wa kuhifadhi taarifa, kumbukumbu na nyaraka kwa njia ya kielektroniki (Digital Records Management and Preservation System) umeanza. Vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kufunga mfumo huu vimenunuliwa na kuwasilishwa katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma ambako ndipo kitakuwa kituo kikuu cha Mfumo. Mkandarasi anatarajiwa kuanza kufunga vifaa hivyo ili kazi ya kuingiza nyaraka katika mfumo ianze;

ii. Kuchambua, kuorodhesha na kuhamisha kumbukumbu kutoka katika baadhi ya Taasisi za Serikali kwenda kwenye Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma. (Makasha 473 za iliyokuwa Kamati ya Ukombozi wa Bara la Afrika kutoka Jeshi la Wananchi Tanzania, Makasha 808 kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Makasha 295 kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Makasha 583 kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Makasha 291 Kutoka Wizara ya nishati na Madini, Makasha 449 kutoka Wzara ya Fedha na Mipango Makasha 1,291 kutoka TASAF, Makasha 138 kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Makasha 1,130 kutoka Mamlaka ya Chakula na Dawa) kazi hiyo ni endelevu;

iii. Machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya Nchi yetu kutoka katika Taasisi za Umma na watu binafsi yamekusanywa. Machapisho haya ni pamoja na Taarifa rasmi za Bunge (Hansards), Ripoti, Hotuba, Majarida, Sera kutoka katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali;

iv. Kukusanya na kufanyia ujalidi magazeti 989 kutoka makampuni ya Business Times, Daily News, Habari leo, Nipashe, Mwanachi, The Guardian na Majira;

v. Waraka wa utekelezaji (implementation Circular) wa majukumu ya kuanzishwa na kuendeshwa Maktaba na Makumbusho ya Marais Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umeandaliwa;

vi. Watafiti 72 wamehudumiwa, kati ya watafiti hao 39 ni wa ndani na watafiti 33 ni wa nje. Idadi ya majalada yaliyosomwa ni 413;

vii. Kutambua na kuratibu ukusanyaji wa vitu na kumbukumbu mbalimbali za Waasisi wa Taifa kumefanyika. Jumla ya vitu na kumbukumbu 2,035 zimetambuliwa, kati yake vitu na kumbukumbu 1,837 zimekusanywa na kuhifadhiwa na Wadau ambao ni pamoja na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Makumbusho ya Taifa, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, KAVAZI la Mwalimu Nyerere na Radio na Televisheni Zanzibar;

viii. Uandaaji wa Makala ya Kihistoria kuhusu Nyumba Kumbukizi aliyowahi kuishi Mwalimu Julius Kambarage-Magomeni. Makala hii inatunza historia ya Nyumba na vitu alivyowahi kutumia Muasisi wakati anaanza harakati zake za kuikomboa nchi yetu;

ix. Kipindi 1 cha Televisheni na kimoja cha Redio viliandaliwa, ili kuelimisha umma kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu Waasisi wa Taifa ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya Mwaka 2004;

x. Mafunzo ya utunzaji kumbukumbu kwa Waratibu wa masuala ya Utunzaji Kumbukumbu katika Taasisi za Umma yamefanyika Dodoma. Jumla ya waratibu 91 walihudhuria mafunzo haya kutoka katika Taasisi mbalimbali za Serikali.

Mafunzo haya yalilenga kuwajengea uwezo wa kusimamia masuala ya utunzaji kumbukumbu katika Taasisi zao;

xi. Taasisi za Umma zimeendelea kusaidiwa kutengeneza miongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu. Katika kipindi hiki jumla ya Taasisi tatu ambazo ni Mkemia Mkuu wa Serikali, Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA), Parastatal Pensions Fund (PPF) na Tanzania Social Action Fund (TASAF) zimesaidiwa kuandaa mwongozo huo; na

xii. Kusimamia na kutoa mwongozo kwa Taasisi za Umma zilizohamia Makao Makuu ya Serikali Dodoma.

USHAURI WA MAFUTA NA GESI (OGAB)

53. *Mheshimiwa Spika,* Ofisi ya Ushauri wa Mafuta na Gesi imeendelea kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uchumi wa mafuta na gesi kwa Baraza la Mawaziri kwa mujibu wa Kifungu cha 7 cha Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015.

54. Mheshimiwa *Spika,* katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Bunge liliidhinisha Shilingi 1,036,239,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2017 Shilingi 141,973,550 fedha za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika.

55. *Mheshimiwa Spika,* katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Ushauri ulitolewa katika masuala yanayohusu uchumi wa mafuta na gesi zikiwemo Sera za Kisekta, Sera ya Uwekezaji, Sheria na Kanuni zinazohusu masuala ya Uchumi wa Mafuta na Gesi na mambo mengine yanayohusiana na Uchumi wa Mafuta na Gesi;

(ii) Utafiti juu ya manufaa ya gesi asili iliyogunduliwa kwa wananchi na Taifa katika kukuza uchumi ulianza mwezi

Julai, 2016 na umekamilika mwezi Februari, 2017. Ripoti ya matokeo ya utafiti huo inaandaliwa;

(iii) Ushauri ulitolewa kuhusu aina ya utaalam unaotakiwa kwenye majadiliano ya mikataba, ukubwa wa timu, mikakati na mbinu zitakazotumika na kushiriki kama waangalizi katika majadiliano ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika Sekta ya Mafuta na Gesi; na

(iv) Kushiriki katika Mikutano mbalimbali iliyofanyika ndani na nje ya nchi yetu ambayo ilijadili masuala yanayohusu mafuta na gesi.

## C. MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2017/18 NA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA

56. *Mheshimiwa Spika,* baada ya kutoa maelezo kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2016/17, sasa naomba kutoa Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2017/18.

57. *Mheshimiwa Spika,* Mipango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/18 kwa Mafungu 20, 30, 32, 33, 67, 94, 09, 04 na 11 imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi wa Mwaka 2015 ya Chama cha Mapinduzi, Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2017/18 pamoja na maeneo muhimu ya kuzingatiwa kama yalivyoainishwa na Serikali ya Awamu ya Tano kama ifuatavyo:-

### OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

(a) Ikulu

58. *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa huduma kwa Rais na familia yake;

(ii) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya uchumi, siasa, masuala ya jamii, sheria, mawasiliano na habari kwa umma, mahusiano ya kikanda, kimataifa na maeneo mengine;

(iii) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu;

(iv) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri;

(v) Kuandaa mkutano wa tathmini wa mwaka kati ya Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na wadau wengine;

(vi) Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara;

(vii) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa na malalamiko ya Watumishi wa Umma na wananchi;

(viii) Kuratibu na kuendesha mikutano 8 ya uratibu wa Maboresho kwa Makatibu Wakuu na Waratibu wa Programu za Maboresho kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa Maboresho katika Sekta ya Umma nchini;

(ix) Kutengeneza na kurusha hewani Vipindi Maalum 60 vya Televisheni, kuchapisha na kutangaza Hotuba na Picha za Mheshimiwa Rais kwenye vyombo vya habari;

(x) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea;

(xi) Kuelimisha watumishi juu ya Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa na utekelezaji wa Mkakati wa Kupambana na Kujikinga na UKIMWI mahali pa kazi pamoja na kuwezesha watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI kupata huduma muhimu za dawa, lishe na ushauri nasaha;

(xii) Kusimamia utoaji wa huduma za afya kwa watumishi kupitia Zahanati ya Ikulu;

(xiii) Kukarabati nyumba 12 za watumishi katika Ikulu Ndogo ya Chamwino na nyumba 1 iliyopo Dodoma Mjini;

(xiv) Kuendelea na ujenzi wa Ikulu mpya Chamwino; na

(xv) Kukarabati majengo ya Ikulu Ndogo za Mwanza, Shinyanga, Mbeya na Moshi.

(b) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)

59. *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, TAKUKURU imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea na ukamilishaji wa uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa unaoendelea pamoja na tuhuma mpya zitakazojitokeza;

(ii) Kuendelea na uendeshaji wa kesi 409 zinazoendelea na mpya zitakazofunguliwa Mahakamani;

(iii) Kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007 ili kujumuisha makosa ya uhujumu uchumi na kutaifisha mali zilizopatikana kwa njia ya Rushwa na Ufisadi;

(iv) Kufanya Utafiti na Udhibiti wa Mianya ya Rushwa katika maeneo ya Vitalu vya Uwindaji, Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa na Tathmini ya Uzingatiaji wa Matumizi ya Mashine za Kielektroniki katika Ukusanyaji wa Kodi;

(v) Kufanya uchambuzi wa mifumo katika Sekta na Idara mbalimbali katika ngazi ya Mikoa na Wilaya;

(vi) Kuweka mikakati kwa kushirikiana na wadau ili kudhibiti mianya ya rushwa na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati hiyo;

(vii) Kufuatilia fedha zinazotolewa na Serikali na Washirika wa Maendeleo katika maeneo yote ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha;

(viii) Kujenga uwezo na uelewa kuhusu rushwa na ufisadi na juhudi za Serikali katika kupambana na rushwa kwa makundi mbalimbali katika jamii kwa kuyashawishi makundi haya kuunga mkono na kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa nchini;

(ix) Kufungua na kuimarisha Klabu za Wapinga Rushwa katika shule za msingi, sekondari na vyuo pamoja na makundi ya vijana wasio shuleni ili kuendelea kujenga jamii inayochukia rushwa;

(x) Kuimarisha mfumo wa TEHAMA katika Taasisi ili kurahisisha na kuwezesha mtiririko mzuri wa majalada, takwimu na mawasiliano kutoka ngazi za Wilaya, Mkoa na Makao Makuu; na

(xi) Ujenzi wa majengo ya Ofisi za TAKUKURU katika Wilaya za Ruangwa, Mpwapwa, Masasi, Ngorongoro, Namtumbo, Manyoni na Chamwino.

(c) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

60. *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

(i) Kukamilisha Uandaaji na utoaji wa Hati za Haki Miliki za Kimila 11,184 katika Halmashauri za Wilaya 14 za Rufiji, Musoma, Sikonge, Chamwino, Kiteto, Meru, Geita, Makete, Kahama, Njombe, Misenyi, Sumbawanga, Misungwi, na Magu;

(ii) Kufanya urasimishaji wa ardhi vijijini katika eneo la Chanjamjawiri, Wilaya ya Chake Chake Pemba na Mahonda, Wilaya ya Kaskazini B Unguja;

(iii) Kutoa mafunzo kuhusu fursa na matumizi bora ya Hati za Haki Miliki za Kimila kwa wakulima 800 waliorasimisha ardhi zao na viongozi 80 wa vyama vya wakulima katika Halmashauri za Wilaya 4 za Mpwapwa, Misungwi, Ngara na Serengeti. Aidha, kwa kushirikiana na Halmashauri husika kusimamia utekelezaji wa Mipango Kazi ya jamii ya vijiji vilivyorasimishwa kwa kuanzisha mashamba darasa na kuunda vikundi vya uzalishaji;

(iv) Kutoa mafunzo kwa Wafanyabishara 3,000 kwa ajili ya urasimishaji wa biashara katika Manispaa ya Dodoma, pamoja na Halmashauri za Wilaya za Urambo na Bariadi. Kwa upande wa Zanzibar, urasimishaji wa biashara utafanyika katika Wilaya ya Kusini Unguja ambapo jumla ya wafanyabiashara 100 watasajiriwa na kupewa mafunzo. Vituo vya Urasimishaji Biashara (One stop centers) vitaanzishwa katika maeneo hayo ili kuwawezesha wafanyabishara kupata

huduma muhimu za usajili, namba ya mlipa kodi, leseni, ushauri wa biashara, pamoja na huduma za kibenki katika sehemu moja;

(v) Kufanya utafiti na tathmini ya ukubwa wa Sekta isiyo rasmi Tanzania Bara na Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi za Taifa za Takwimu Tanzania Bara na Zanzibar;

(vi) Kwa kushirikiana na TAMISEMI, MKURABITA itaratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya majaribio ya Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya katika Manispaa ya Iringa na Halmashauri 2 za Mkoa wa Songwe;

(vii) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya maboresho ya sheria za ardhi na biashara;

(viii) Kukamilisha uandaaji wa hati katika Halmashauri za Miji ya Njombe, Morogoro, Arusha, Tunduma, Iringa, Babati, Miji Midogo ya Tandala na Ikonda Tanzania Bara, ambako urasimishaji ardhi mijini ulifanyika;

(ix) Kufanya urasimishaji wa ardhi mjini katika Wilaya za Chake Chake, Pemba na Unguja Mjini;

(x) Kukamilisha ujenzi wa Masjala za Ardhi za Vijiji 12 katika Halmashauri za Wilaya 5 ambazo ni Mvomero, Manyoni, Nachingwea, Mbinga na Chamwino. Aidha, ujenzi wa Masjala za Ardhi za Vijiji 8 utaendelea na kufikia hatua ya kuezeka katika Halmashauri za Wilaya 8 za Sumbawanga, Kalambo, Meru, Mwanga, Masasi, Mbarali, Moshi na Makete;

(xi) Kununua kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi za MKURABITA lenye ghorofa moja Dodoma. Aidha, taratibu za kumpata mzabuni wa usanifu wa michoro na wa ujenzi zitakamilishwa na kuanza ujenzi; na

(xii) Kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini kuanza urasimishaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini katika maeneo ya Mkoa wa Geita.

(d) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

61. *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

(i) Kufanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo ya Vijiji, Mitaa na Shehia zote ambazo hazikufikiwa katika awamu ya kwanza. Utambuzi na uandikishaji huu unategemea kuwafikia kaya za walengwa 355,000 katika Vijiji, Mitaa na Shehia 5,690;

(ii) Kuendelea kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini zipatazo 1,100,000 katika vipindi 6 vya mizunguko ya malipo katika Halmashauri zote za Tanzania Bara pamoja na Unguja na Pemba, Zanzibar. (Uhawilishaji wa fedha utafanywa kwa kufuata Kalenda ya Malipo ya kila baada ya miezi miwili);

(iii) Kuziondoa katika Mpango, kaya za walengwa wenye hali zilizoboreka baada ya kupokea ruzuku kwa muda wa miaka mitatu mfululizo kwa kuzingatia taratibu na miongozo iliyoelekezwa katika Mpango;

(iv) Kuendelea kufanya uhakiki wa walengwa wanaostahili kunufaika na Mpango na kuwaondoa wasiostahili kuwemo kwa sababu mbalimbali;

(v) Kutoa ajira za muda kwa jumla ya kaya za walengwa 298,970 ambazo zitahusika katika utekelezaji wa kazi za ajira za muda kwa Kaya Maskini. Walengwa hawa watatoka katika Halmashauri 42 pamoja na Unguja na Pemba;

(vi) Kuendeleza utekelezaji wa Mkakati na Miongozo ya Kuweka Akiba na kuwekeza katika maeneo ya utekelezaji. Wawezeshaji 200 watapatiwa mafunzo ya kuunda vikundi endelevu vya kuweka akiba kwa kaya za walengwa. Jumla ya vikundi 26,162 vya walengwa vitaundwa, kupewa mafunzo na vitendea kazi. TASAF imepanga kutoa ruzuku kwa vikundi 34,000 vitakavyofanya vizuri;

(vii) Kutekeleza jumla ya miradi 143 ya afya, elimu, ujasiliamali na barabara za vijijini chini ya Mpango wa Kuendeleza Miundombinu. Wafanyakazi 850 wa Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa na Wajumbe wa Kamati 143 za Usimamizi za Jamii watapewa mafunzo juu ya namna ya kutekeleza na kusimamia miradi;

(viii) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ya utunzaji wa kumbukumbu za walengwa, uendeshaji na utoaji taarifa ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Mpango hususan kuimarisha mawasiliano kati ya maeneo ya utekelezaji na TASAF Makao Makuu;

(ix) Kufanya utafiti shirikishi katika maeneo mbalimbali ya kijamii na kiuchumi ili kubaini fursa na vikwazo katika kufikia lengo la jamii kujipatia maendeleo. Hii itahusisha kukusanya takwimu mbalimbali katika ngazi za jamii kwa ajili ya utafiti huo;

(x) Kujenga uwezo wa watumishi katika ngazi mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na TASAF Makao Mkuu, Mikoa, Halmashauri na jamii ili kuweza kusimamia na kutekeleza shughuli za Mpango kwa ufanisi; na

(xi) Kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini za shughuli za Mpango pamoja na matumizi ya rasilimali ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika ngazi zote za utekelezaji wa Mpango. Shughuli hii pia itahusisha kufanya tathmini ya kwanza ya

Mpango ili kupima ni kwa kiasi gani Mpango umeweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

(e) Taasisi ya UONGOZI

62. *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

(i) Kutoa mafunzo ya "Stashahada ya Uzamili katika Uongozi" (Post Graduate Diploma in Leadership), kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi katika maeneo ya kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimali watu na rasilimali nyingine;

(ii) Kutekeleza Programu ya kuwajengea uwezo wataalam wa Wizara na Taasisi za Serikali wa kufanya majadiliano ya mikataba yenye thamani kubwa na namna ya kuunda timu madhubuti za majadiliano;

(iii) Kutoa kozi 18 za mafunzo ya muda mfupi na ushauri wa kitaalam kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi katika maeneo ya uongozi na maendeleo endelevu, kutokana na mahitaji na maombi ya walengwa;

(iv) Kuandaa mikutano 4 ya Kimataifa na Kikanda, 3 ya Kitaifa na 10 ya faragha juu ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;

(v) Kuandaa vipindi vya televisheni 18 vitakavyoshirikisha viongozi waandamizi na wataalam mbalimbali ndani na nje ya nchi, juu ya Uongozi na Maendeleo Endelevu. Vipindi hivi vitarushwa kwenye runinga, tovuti na mitandao ya kijamii na kuonekana katika Bara zima la Afrika;

(vi) Kufanya tafiti 9 zinazohusu masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;

(vii) Kuandaa chapisho litakaloelezea maisha na uzoefu wa Kiongozi maarufu Mstaafu;

(viii) Kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo yanayohusu masuala ya uongozi na maendeleo endelevu pale utakapohitajika;

(ix) Kutekeleza Programu Jumuishi juu ya Usimamizi wa Rasilimali za Taifa katika sekta ya uziduaji; na

(x) Kushiriki katika uendeshaji wa Kituo cha Tathmini kwa lengo la kuboresha mfumo wa uteuzi wa viongozi wa kati na waandamizi katika Utumishi wa Umma.

(f) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)

63. *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea umepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kutoa mikopo 3,600 kwa walengwa yenye thamani ya Sh. 2,415,000,000;

(ii) Kutoa mafunzo ya awali kwa walengwa 4,000 na mafunzo endelevu kwa wanufaika 2,000;

(iii) Kufanya tafiti na kutoa huduma katika Mikoa ya Dodoma (Wilaya ya Dodoma), Kagera (Wilaya ya Bukoba Vijijini) na Iringa (Wilaya ya Kilolo); na

(iv) Kuendelea kujenga uwezo wa watendaji wa Mfuko ili kutoa huduma bora kwa wateja.

64. *Mheshimiwa Spika,* ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Fungu 20 Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba Shilingi 16,267,586,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha,

Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inaomba kuidhinishiwa Shilingi 747,885,035,000. Kati ya fedha hizi, Shilingi 368,314,145,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 379,570,890,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA WAKALA ZILIZO CHINI YAKE

a) Menejimenti ya Utumishi wa Umma

65. *Mheshimiwa Spika,* Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika mwaka wa fedha wa 2017/18 itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa.

66. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kujenga uwezo wa Serikali katika kuratibu utungaji na utekelezaji Sera unaowiana (Policy Coherence) ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

(ii) Kuanzisha na kuhuisha Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Taasisi za Umma kulingana na mahitaji ya Serikali ya Awamu ya Tano ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi;

(iii) Kuendelea kutoa vibali vya uhamisho na uteuzi kwa watumishi wanaopendekezwa na waajiri mbalimbali kushika nyadhifa za uongozi. Aidha, Ofisi yangu itaendelea kuwezesha uhamisho wa watumishi miongoni mwa waajiri na kushughulikia maombi ya vibali vya likizo bila malipo,

kuazimwa na kushikizwa yanayowasilishwa na waajiri na watumishi;

(iv) Kuendelea kushughulikia malalamiko yatokanayo na ukiukwaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya Utumishi wa Umma na kuchukua hatua stahiki kwa waajiri wanaolalamikiwa kwa kutozingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu hizo;

(v) Kuboresha michakato ya utoaji wa huduma na kuimarisha usimamizi wa mifumo na viwango vya utendaji kazi kwa kufanya ufuatiliaji na kutoa ushauri wa kitaalamu katika Taasisi za Serikali;

(vi) Kuratibu tathmini ya utendaji kazi wa Wakala za Serikali ili kubaini tija iliyopatikana na changamoto za uendeshaji wa vyombo hivi vya Serikali;

(vii) Kuratibu mapendekezo mbalimbali ya kuboresha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ili kuendelea kuhuisha mfumo uwe madhubuti uliooanishwa ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa na matokeo yatakayosaidia kufanya maamuzi na kuboresha sera na mikakati ya Serikali kwa ujumla;

(viii) Kusimamia na kuratibu fursa za mafunzo kwa ajili ya kujenga uwezo wa Watumishi wa Umma kufanya kazi kwa ufanisi;

(ix) Kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na kanuni mbalimbali za mafunzo kwa Watumishi wa Umma;

(x) Kuziwezesha Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo (Training Needs Assessment) ili kuhakikisha kwamba Programu za mafunzo zinazotolewa zinakidhi mahitaji halisi ya mafunzo ya Taasisi;

(xi) Kuziwezesha Taasisi za Umma 10 zinazohitaji kuandaa mipango ya Rasilimali watu na Urithishanaji Madaraka;

(xii) Kuandaa mwongozo wa kuwezesha Taasisi za Umma kuwa na Mpango wa Rasilimali watu wa muda wa kati na muda mrefu katika Utumishi wa Umma;

(xiii) Kuhimiza watanzania wenye sifa kuomba kazi katika mashirika ya kimataifa na kikanda pindi nafasi zinapojitokeza;

(xiv) Kuendelea kufanya vikao vya kazi na Sekretarieti za Mikoa yote na Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia huduma ya 'Video Conference' pamoja na kusambaza mwongozo wa matumizi ya huduma hiyo katika Taasisi za Serikali;

(xv) Kuendelea kuboresha Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Malipo ya Mishahara katika ngazi zote za Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala ya Serikali; Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na kuhuisha mfumo huo kuendana na mahitaji ya sasa na teknolojia iliyopo;

(xvi) Kuendelea na utekelezaji wa mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Malipo ya Mishahara katika Idara za Kilimo na Mifugo kwa kutoa mafunzo kwa watumishi wa Idara hizo, na kufuatilia utekelezaji wa mfumo huo katika Idara za Afya na Elimu katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa;

(xvii) Kuratibu Utekelezaji wa Miradi inayohusiana na Serikali Mtandao chini ya Programu ya Miundombinu ya Mawasiliano ya Kikanda, kwa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika (RCIP);

(xviii) Kuendelea na usanifu na uidhinishaji wa Programu ya Uboreshaji wa Utumishi wa Umma;

(xix) Kusimamia ajira za Watumishi wa Umma ambapo katika mwaka wa fedha wa 2017/18 Serikali inatarajia kuajiri watumishi kwa kuzingatia vipaumbele na kuimarisha maeneo yenye upungufu mkubwa;

(xx) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa matumizi sahihi ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara;

(xxi) Kufanya uhakiki wa mahitaji sahihi ya rasilimaliwatu katika Mikoa 5 na kutoa mafunzo kwa Maofisa Rasilimaliwatu 30 kutoka Taasisi za Umma;

(xxii) Kufanya Kampeni na ufuatiliaji wa uzingatiaji wa Maadili utekelezaji wa Ahadi za Uadilifu na uzingatiaji wa maadili katika (Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali) 20, Sekretarieti za Mikoa 2 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 13;

(xxiii) Kuhuisha Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2005;

(xxiv) Kuratibu, kusimamia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo wa Anuai za Jamii, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa (MSY) katika Utumishi wa Umma;

(xxv) Kufuatilia utekelezaji wa Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu wa Mwaka 2008;

(xxvi) Kujenga uelewa wa Mfumo wa Mikataba ya Utendaji Kazi kwa Viongozi wa Kisiasa na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma;

(xxvii) Kuwezesha Menejimenti za Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, na Majopo ya Kitaalamu ya Serikali kufanya majadiliano juu ya utekelezaji wa Mikataba ya Utendaji Kazi;

(xxviii) Kuzijengea uwezo Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Mashirika ya Umma juu ya uandaaji na utekelezaji wa Mikataba ya Utendaji Kazi; na

(xxix) Kukamilisha kuandaa Sera ya Serikali Mtandao pamoja na Mpango Mkakati wake wa Utekelezaji, na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miongozo ya Serikali Mtandao katika taasisi za Umma;

b) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)

67. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa 2017/18, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma kwa Watumishi 840;

(ii) Kutoa Mafunzo ya Uongozi, Menejimenti na Utawala kwa Watumishi wa Umma 2,790;

(iii) Kutoa Mafunzo ya Awali katika Utumishi wa Umma kwa Watumishi wa Umma 2,010;

(iv) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 15,810 katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili, Kompyuta, Utunzaji wa Fedha za Umma, na Menejimenti ya Rasilimali Watu, Usimamizi wa Manunuzi ya Umma, Uongozi na Utawala Bora;

(v) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Taasisi za Umma 21;

(vi) Kufanya utafiti katika maeneo 6 yanayolenga kuboresha Utumishi wa Umma;

(vii) Kuanzisha Shahada ya Kwanza katika kozi za Uhazili na Utunzaji wa Kumbukumbu;

(viii) Kuandaa machapisho mbalimbali kama vile majarida, vitabu, na makala za kitaalamu katika Utumishi wa Umma katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala;

(ix) Kugharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 30 wa Chuo cha Utumishi wa Umma katika ngazi zifuatazo: 17 Shahada ya Uzamivu, 09 Shahada ya Uzamili na 04 Shahada ya Kwanza;

(x) Kugharamia mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 80 wa Chuo cha Utumishi wa Umma katika maeneo ya Uongozi na Utawala Bora katika Utumishi wa Umma na maeneo mengine kulingana na taaluma zao;

(xi) Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la ghorofa 2 litakalotumika kwa ajili ya madarasa, maktaba na ofisi katika Kampasi ya Tabora na kufanya ukarabati wa Hostel;

(xii) Kufanya maandalizi ya upanuzi wa maeneo au kampasi za kutolea mafunzo katika mikoa ya Mwanza, Singida na Dodoma kwa kuandaa Mpango Kabambe (Master Plan) wa eneo la Singida, kukamilisha umilikishwaji wa eneo la Mwanza na kununua eneo mkoani Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania na kukarabati jengo la Chuo lililopo Dodoma;

(xiii) Kufanya ukarabati wa mfumo wa umeme na kuweka mfumo wa mawasiliano ya ndani ya kielektroniki (LAN) katika majengo ya Kampasi ya Dar es Salaam; na

(xiv) Kuandaa mpango kazi wa utekelezaji wa ushirikiano na Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo.

c) Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA)

68. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa mafunzo kwa washiriki 2,500 katika maeneo ya uongozi, utawala bora, maadili, anuai za jamii, mazingira, kupunguza umasikini, Afya na TEHAMA;

(ii) Kuongeza ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi ili kutoa mafunzo kwa kutumia teknolojia za kisasa na kwa gharama nafuu;

(iii) Kukuza mtandao wa Wakala kikanda ili kuwafikia wateja walioko mikoani kwa urahisi;

(iv) Kununua vitendea kazi kwa ajili ya Wakala ili kuongeza uwezo wa kutoa huduma bora zinazoendana na ukuaji wa mahitaji;

(v) Kufanya usanifu kwa ajili ya maandalizi ya kujenga ofisi za Wakala Dodoma;

(vi) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi 18 wa Wakala ili kuwaongezea uwezo wa utendaji kazi;

(vii) Kuratibu mikutano ya kazi ya Wizara, Mamlaka za Serikaliza Mitaa, Idara, Wakala na taasisi nyingine za serikali kwa kutumia huduma ya daraja-video (bridging services) na kutoa ushauri wa kitaalamu; na

(viii) Kufanya utafiti na majaribio ya teknolojia rafiki na rahisi za mawasiliano ya video na mafunzo na kuziboresha.

d) Wakala ya Serikali Mtandao (eGA)

69. *Mheshimiwa Spika,* Katika kipindi cha mwaka wa fedha cha 2017/18, Wakala ya Serikali Mtandao inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea na usimamizi na uendeshaji wa Vituo vya Kuhifadhi Taarifa na Mifumo ya TEHAMA ya Serikalini (Government Data Centres) kwa lengo la kuongeza usalama, kupunguza gharama na kujikinga na Majanga;

(ii) Kuunganisha Taasisi 80 kwenye Mfumo wa Pamoja na Salama wa Barua Pepe wa Serikali na hivyo kuwa na idadi ya taasisi 281 zinazotumia mfumo salama wa mawasiliano serikalini na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi;

(iii) Kutengeneza mfumo wa kuwezesha ubadilishanaji taarifa ili kuondoa udurufu, kupunguza gharama na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma;

(iv) Kukamilisha kazi ya ujenzi wa Mfumo wa Kielekroniki wa Masijala (e-Office) na kusambazwa kwenye Wizara zote na taasisi zitakazokuwa zimeunganishwa kwenye Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali (Government Network) ili kuendelea kurahisisha ubadilishanaji wa nyaraka na utoaji wa maamuzi Serikalini.

(v) Kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za Serikali hususani Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mfumo Mkuu wa Kusimamia Malipo na Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali Kieletroniki (Government Payment Gateway) utakamilishwa na kuanza kutumiwa rasmi na taasisi mbalimbali za Serikali;

(vi) Kuongeza matumizi ya pamoja ya Miundombinu na Mifumo ya TEHAMA kwa kuongeza matumizi ya Miundombinu iliyopo. Lengo ni kuhakikisha angalau Taasisi 100 za Serikali

zinatumia rasilimali hizi pamoja na kuongeza huduma za Serikali zinazotolewa kupitia miundombinu hii;

(vii) Kutoa mafunzo ya Serikali Mtandao kwa Viongozi, Wasimamizi wa TEHAMA na Watumishi wa kada mbalimbali kutoka taasisi 150 ili kuongeza uelewa na uwezo wa Taasisi za Umma katika kutumia TEHAMA, kuongeza ufanisi wa kiutendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi;

(viii) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya Serikali Mtandao kwa njia mbalimbali ikiwemo vipindi vya runinga, redio, machapisho na kwenye mitandao;

(ix) Kutoa ushauri wa kitaalam na msaada wa kiufundi kwenye maeneo ya TEHAMA kwa Taasisi 300 za Serikali;

(x) Kukamilisha kuunganisha Taasisi 77 (Hospitali za Mikoa 19, Ofisi za Halmashauri 38 na Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa 20) za Serikali za Mitaa kwenye Mfumo wa Mawasiliano wa Serikali;

(xi) Kuwezesha watumishi 40 wa Wakala kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi, 10 mafunzo ya kitalaam (professional training) na watumishi 2 mafunzo ya muda mrefu; na

(xii) Kutoa elimu kwa watumishi wa Wakala kuhusu VVU na UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa na mapambano dhidi ya rushwa.

70. *Mheshimiwa Spika,* ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kwa ufanisi, Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Shilingi 33,695,038,000. Kati ya fedha hizi, Shilingi 26,695,038,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 7,000,000,000 kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

71. *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:

(i) Kupokea Tamko la Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na Madeni linalopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(ii) Kupokea na kushughulikia malalamiko na taarifa za ukiukwaji wa Maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutoka kwa wananchi;

(iii) Kuchunguza tuhuma yoyote ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma dhidi ya Viongozi wa Umma;

(iv) Kufanya uhakiki wa matamko ya Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma 1,000;

(v) Kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma;

(vi) Kuelimisha Viongozi wa Umma na Wananchi kwa ujumla kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Hati ya Ahadi ya Uadilifu;

(vii) Kuandaa taarifa ya Mwaka ya utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti na kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(viii) Kuanzisha na kuendeleza Klabu za Maadili katika shule na vyuo nchini; na

(ix) Kuanzisha mchakato wa kutumia mfumo wa ujazaji wa fomu za matamko ya rasilimali na madeni kwa viongozi wa umma kwa njia ya mtandao (online application) baada ya kukamilika

kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Taarifa za Kimaadili (Ethics Management Information System – EMIS).

72. *Mheshimiwa Spika,* katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaomba kuidhinishiwa Shilingi 8,640,422,004. Kati ya fedha hizi Shilingi 6,990,422,004 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 1,650,000,000 ni fedha za nje kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

73. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka cha fedha wa 2017/18, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kusimamia na kuendesha mchakato wa ajira ili kuwezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;

(ii) Kuimarisha kanzidata ya kutunza taarifa za waliopangiwa vituo vya kazi, taarifa za kada zenye wataalam wenye ujuzi maalum (rare profession) na taarifa za wahitimu wa vyuo vikuu nchini;

(iii) Kuendelea kufanya utafiti kwa waajiri na wadau mbalimbali ikiwa ni hatua ya kupata mrejesho wa utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa michakato ya ajira pamoja na utendaji wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

(iv) Kuboresha mfumo wa kielektroniki wa maombi ya kazi (recruitment portal) ili uwasiliane na mifumo mingine kwa lengo la kuwapata watumishi wenye sifa;

(v) Kuendelea kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira Zanzibar ili kurahisisha mchakato wa ajira kwa ajira za Muungano;

(vi) Kwa kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao, kuendelea kuboresha na kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa kuendesha mchakato wa ajira na utunzaji kumbukumbu za wasailiwa na wataalam mbalimbali na mfumo wa kutuma ujumbe mfupi wa simu za kiganjani (bulk sms);

(vii) Kushiriki kama Wataalam waalikwa kwenye usaili unaoendeshwa na Taasisi zinazotumia Sheria zilizokasimiwa kwao;

(viii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani ya nchi kwa watumishi 5. Aidha, mafunzo pia yatatolewa kwa watumishi wengine kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wa watumishi hao;

(ix) Kuboresha mifumo ya uendeshaji wa usaili kwa kutumia mbinu za kisasa, ikiwemo matumizi ya "psychometric tests";

(x) Kutoa taarifa na elimu kwa umma ili kukuza uelewa katika shughuli zinazotekelezwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

(xi) Kusimamia mashauri yahusuyo waombaji wa ajira wanaogushi vyeti; na

(xii) Kuimarisha miundo mbinu ya TEHAMA itakayosaidia uboreshaji wa utendaji kazi wa Taasisi.

74. *Mheshimiwa Spika,* katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha wa 2017/18, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa Jumla ya Shilingi 3,115,975,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, Shilingi 2,365,975,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 750,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

TUME YA UTUMISHI WA UMMA

75. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Tume ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kufanya Ukaguzi wa kawaida kwa Taasisi 150 na Ukaguzi Maalum kwa Taasisi 10 kuangalia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kufanya mikutano ya kisheria ya Tume kujadili na kutolea uamuzi taarifa za ukaguzi, rufaa, malalamiko na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakavyopokelewa;

(iii) Kuelimisha Taasisi za Umma na Watumishi wa Umma kuhusu majukumu ya Tume na utekelezaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma kupitia, ziara za Makamishna, vikao vya kazi, vyombo vya habari, machapisho na Tovuti;

(iv) Kuandaa Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2016/17 na kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Rais;

(v) Kutoa elimu na mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi wapya 24 wa Tume;

(vi) Kutoa huduma kwa watumishi wa Tume wanaoishi na VVU na UKIMWI; na

(vii) Kutoa elimu kwa watumishi wa Tume kuhusu VVU, UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa na mapambano dhidi ya rushwa.

76. *Mheshimiwa Spika*, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Fungu 94 Tume ya Utumishi wa Umma

inatarajia kutumia kiasi cha Shilingi 4,909,515,670 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

## BODI YA MISHAHARA NA MASILAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

77. *Mheshimiwa Spika,* kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2017/18, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kufanya utafiti wa namna ya kutoa motisha kwa kuzingatia utendaji katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kutoa elimu kwa wadau kuhusu vigezo vinavyotumika kupanga mishahara na masilahi katika Utumishi wa Umma;

(iii) Kuandaa taarifa za gharama za chini za maisha kama msingi wa kukadiria kiwango cha mshahara wenye staha; na

(iv) Kuwajengea uwezo wajumbe 7 na watumishi 20 wa Bodi kuhusu masuala ya mishahara na masilahi.

78. *Mheshimiwa Spika,* ili kutekeleza Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa Shilingi 1,721,977,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

## IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

79. *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa itatekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuendelea kukagua, kuchambua na kuhamisha kumbukumbu tuli kutoka katika Taasisi za Umma 25 na

Mamlaka za Serikali za Mitaa 18 kwenda Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu, Dodoma;

ii. Kusaidia taasisi za umma 6 kutengeneza miongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu;

iii. Kujenga uwezo wa taasisi za umma katika usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali kwa kuandaa mikutano kazi kwa Menejimenti za taasisi za umma na Mafunzo kazi kwa Waratibu na watunza kumbukumbu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utunzaji wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za serikali;

iv. Kukusanya taarifa na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya nchi yetu kutoka taasisi za umma na watu binafsi;

v. Kutambua, kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa;

vi. Kuweka na kuhuisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali 20 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 18 ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma Serikalini;

vii. Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika usimamizi wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Taifa kwa kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka katika teknolojia ya kisasa kwa kuanzisha Mfumo wa Kidijitali wa Kuhifadhi Nyaraka (Digital Records Management and Preservation System) ili kurahisisha upatikanaji na kulinda nakala halisi;

viii. Kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Masjala (e-Filing) kwa lengo la kuboresha huduma, kupunguza gharama na kurahisisha zoezi la Serikali kuhamia Dodoma;

ix. Kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu katika Kanda ya Ziwa- Mwanza;

x. Kuimarisha uwezo wa utendaji wa watumishi wa Idara; na

xi. Kufanya uhakiki (appraisal) wa kumbukumbu tuli za taasisi 3 za umma zilizohifadhiwa katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma ili kubaini zenye umuhimu wa kuendelea kuhifadhiwa na zile ambazo umuhimu wake umekoma ili kuteketezwa.

80. *Mheshimiwa Spika,* katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa inaomba kuidhinishiwa Shilingi 4,375,726,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, Shilingi 2,375,726,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 2,000,000,000 ni kwa ajili ya mradi wa Maendeleo.

OFISI YA RAIS, USHAURI WA MAFUTA NA GESI (OGAB)

81. *Mheshimiwa Spika,* katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

(i) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa Baraza la Mawaziri katika masuala yanayohusu uchumi wa mafuta na gesi zikiwemo Sera za Kisekta, Sera ya Uwekezaji, Sheria na Kanuni zinazohusu masuala ya uchumi wa mafuta na gesi na mambo mengine yanayohusiana na uchumi wa mafuta na gesi;

(ii) Kufanya tafiti mbalimbali za uchumi wa mafuta na gesi na kulishauri Baraza la Mawaziri ili kuchochea maendeleo endelevu kwa faida ya Watanzania wote;

(iii) Kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu aina ya utaalam utakaohusika kwenye majadiliano ya mikataba, ukubwa wa timu ya majadiliano, mikakati na mbinu zitakazotumika na kushiriki kama waangalizi katika majadiliano ya uwekezaji wa kimkakati katika sekta ya mafuta na gesi; na

(iv) Kuwajengea uwezo wataalam wa ushauri wa mafuta na gesi kwa kuwapa mafunzo nje na ndani ya nchi.

82. *Mheshimiwa Spika,* ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Ofisi ya Rais, Ushauri wa Mafuta na Gesi inaomba kuidhinishiwa Shilingi 711,073,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

MAJUMUISHO

83. *Mheshimiwa Spika,* Mipango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2017/18 ya mafungu yaliyotajwa imezingatia vipaumbele na matakwa ya Serikali ya Awamu ya Tano yenye kusudio la kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika Utumishi wa Umma ili kuondokana na matumizi mabaya ya rasilimali, ukiukwaji wa maadili ya uongozi na urasimu katika utoaji wa huduma kwa wananchi na kuwa mifumo thabiti ya usimamizi wa utekelezaji. Tunaamini kuwa Utumishi wa Umma uliotukuka ni chachu ya maendeleo kwa Taifa lolote duniani. Hivyo nasi pia tumejipanga kikamilifu kuhakikisha kuwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zake inatoa mchango wake maridhawa katika kufikia malengo yetu kama Taifa na kuiwezesha Nchi yetu kuwa ya uchumi wa kati ifikapo Mwaka 2025.

84. *Mheshimiwa Spika,* napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaunga mkono kwa dhati juhudi za Mheshimiwa Rais za kupiga vita rushwa, ubadhirifu wa mali ya Umma na ufisadi. Tunaunga mkono hatua stahiki zinazochukuliwa na viongozi katika ngazi mbalimbali ili kurejesha nidhamu ya Utumishi wa Umma na kuboresha huduma kwa wananchi. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge na watu wenye mapenzi mema kwa Nchi yetu waendelee kuunga mkono juhudi hizi. Tumeanza kuona mafanikio lakini bado tunayo kazi kubwa ya kufanya mbele yetu. Aidha, tunaunga mkono kwa nguvu zote uamuzi wa Serikali

kuhamia Dodoma, kwa kuanzia Ofisi yangu imeshaanza kutoa huduma ikiwa Makao Makuu kama ilivyoamuliwa.

85. *Mheshimiwa Spika,* baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 na mipango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha wa 2017/18, naomba kuwasilisha maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

a. Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu

| | | |
|---|---|---|
| i. Matumizi ya Kawaida | Sh. | 16,267,586,000 |
| Jumla | Sh. | 16,267,586,000 |

b. Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri

| | | |
|---|---|---|
| i. Matumizi ya Kawaida | Sh. | 368,314,145,000 |
| ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 379,570,890,000 |
| Jumla | Sh. | 747,885,035,000 |

c. Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma

| | | |
|---|---|---|
| i. Matumizi ya Kawaida | Sh. | 26,695,038,000 |
| ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 7,000,000,000 |
| Jumla | Sh. | 33,695,038,000 |

d. Fungu 33: Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma

| | | |
|---|---|---|
| i. Matumizi ya Kawaida | Sh. | 6,990,422,004 |
| ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 1,650,000,000 |
| Jumla | Sh. | 8,640,422,004 |

e. Fungu 67: Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma

| | | |
|---|---|---|
| i. Matumizi ya Kawaida | Sh. | 2,365,975,000 |
| ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 750,000,000 |
| Jumla | Sh. | 3,115,975,000 |

f. Fungu 94: Tume ya Utumishi wa Umma

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | Sh. | 4,909,515,670 |
| Jumla | Sh. | 4,909,515,670 |

g. Fungu 09: Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa

Umma

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | Sh. | 1,721,977,000 |
| Jumla | Sh. | 1,721,977,000 |

h. Fungu 04: Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | Sh. | 2,375,726,000 |
| Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 2,000,000,000 |
| Jumla | Sh. | 4,375,726,000 |

j. Fungu 11: Ofisi ya Ushauri ya Mafuta na Gesi Asilia

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | Sh. | 711,073,000 |
| Jumla | Sh. | 711,073,000 |

86. *Mheshimiwa Spika*, Jumla kuu ya Bajeti ninayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2017/18, ni kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | Sh. | 430,351,457,674 |
| Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 390,970,890,000 |
| Jumla kuu kwa Mafungu yote | Sh. | 821,322,347,674 |

87. *Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge*, mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaidhinisha.

88. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja.

ANGELLAH J. KAIRUKI (MB)
WAZIRI WA NCHI
OFISI YA RAIS - MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA